
**Chongolo** aonya 'uchawa', maslahi binafsi UVCCM

UKURASA 5



**Wagonjwa** figo waongezeka kwa asilimia 72 Mloganzila

UKURASA 7



ama

ALHAMISI JUNI 8, 2023

AFYA NA MAZINGIRA

Ukurasa 12

Watoto wanaotamani udaktari wapelekwa kuzuru Muhimbili

Ukurasa 13

Dawa za kulevya zinavyobaki sumu ya afya jamii nchini, hadi duniani

Ukurasa 14

SUA yabuni kifaa Smart TB, cha kumsaka mgonjwa asiyepo kliniki

UTEKELEZAJI MBIU YA RAIS SAMIA...

Wizara ya Afya harakati zimepamba teknolojia kukusanya mazao damu

Na Yasmine Protace

• Njia mpya ya kuwezesha ziada ya benki
• Kila hospitali rufani kuwa na kituo chake

INAFAHAMIKA, damu ni muhimu kwa binadamu na inapaswa kuwamo mwilini ikiwa safi na salama. Hiyo ndiyo sababu katika hospitali kubwa ni kanuni sasa kuwa na benki ya damu na kitaifa kuna vituo maalum vya benki ya damu, kwa ngazi tofauti hata kufikia kwenye kanda.

Kwa mujibu wa Mpango wa Taifa wa Damu Salama, kunakusanywa damu kutoka kwa wachangiaji wa hiari ikifanyika kwa njia kuu mbili; uchangiaji wa damu nzima, pia kuchangia mazao mahsusi ya damu (apheresis donation).

Katika eneo hilo la pili, mchangiaji anatoa damu kwa sehemu maalum kama vile katika tafsiri ya kitaalamu; chembe sahani (platelets), sehemu ya majimaji ya damu (plasma) au seli nyekundu (red blood cells).

Damu Salama, ambayo imeanza utekelezaji wa kuongeza wigo wa kutengeneza mazao damu kwa kuhusisha hospitali za rufani mikoa na kanda.

Anasema, awali kazi hiyo ilifanyika katika vituo vya Damu Salama-Kanda. Hadi sasa, hospitali zilizokwishajengewa uwezo wa kutengeneza mazao ya damu zinatajwa ni za mikoa ya Geita, Simiyu, Iringa na Arusha-Mount Meru.

Pia, Dk. Juma anataja katika orodha hiyo, vituo vikubwa vya afya kitaifa, zimo hospitali za Benjamin Mkapa, pia zingine za Dar es Salaam; Mloganzila, Taasisi ya Mifupa-MOI, CCBRT na Hospitali ya Taifa Muhimbili, kukifanyikia uzalishaji wa moja kwa moja wakati mtu anapochangia damu, kulingana na mahitaji ya kituo.

UKURASA 11

Alhamisi Juni 29, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581356

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



# 'ULAJI WA SERIKALINI'

• **Kamati** ya Bunge yashtuka waliotafuna mabilioni waadhibiwa kwa barua ya onyo... *Ukurasa 2,4&8*




## YALIYOMO

UKURASA WA 4

**ALIYESHTAKIWA TUHUMA KUUA MCHUNGAJI KUNYONGWA HADI KUFA**

HATIMAYE aliyeshtakiwa kwa kumuua mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la...

UKURASA WA 17

**MAKAMU WA RAIS ATAJA CHANZO MIGOGORO YA KISIASA ZANZIBAR**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Othman Masoud Othman amesema jamii...

## Eneo la DART Gerezani kuwa la kimataifa

UKURASA 4



# Waziri Mkuu: Bandari isitugawe

• **Atoa** ufafanuzi mapato, muda wa mkataba... *Endelea ukurasa 3*

**MICHEZO** BANGALA AWASHUSHA PRESHA MASHABIKI UK.24 **KATUNI** UK.6

# 'Ulaji wa serikalini'

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) imewasilisha taarifa yake bungeni kuhusu utekelezaji wa maazimio ya Bunge ya hoja za ukaguzi kwa mwaka 2020/21 na kubainisha kutochukuliwa hatua stahiki watumishi waliobainika kufuja mabilioni ya shilingi.

Ni angalizo la kamati hiyo, ikishangazwa na hesabu zenye utata kwa hesabu ya Sh. trilioni kadhaa, ikigusa taasisi nyeti zinazoshikilia uchumi wa nchi, hali kadhalika misamaha tata ikiwaangukia wanaoonyooshewa kidole cha moja kwa moja kutokana na ukaguzi wa hesabu uliofanywa.

Vilevile, kamati hiyo imesema itafanya uchambuzi wa kina wa taarifa za ukaguzi maalum anaofanya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) wa Mfuko wa Tozo na Tuzo wa Jeshi la Polisi.

Akiwasilisha taarifa ya kamati hiyo bungeni juzi, Mwenyekiti wa PAC, Naghenjwa Kaboyoka, alisema katika kikao cha Bunge cha Novemba 2022, Bunge liliazimia serikali ichukue hatua za kisheria kwa watumishi 32 wa Idara ya Uhamiaji waliotajwa kuhusika katika mauzo ya stika viza bandia katika Uwanja wa Kimataifa wa Ndege wa Kilimanjaro (KIA) kwa kuzingatia uhusika wa kila mmoja kwa kuiba fedha za umma Sh. bilioni 2.48.

Alisema taarifa za serikali imefafanua kwamba Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi awali mwaka 2019 ilitoa taarifa watumishi hao walifunguliwa shauri la uhujumu uchumi Na. 5/2019 katika Mahakama ya Hakimu Mkazi mjini Moshi mkoani Kilimanjaro, baadaye liliondolewa mahakamani tarehe 12 Julai, 2021 baada ya Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kutokuwa na nia ya kuendelea na shauri hilo.

Alisema wizara iliwasiliana na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa barua yenye Kumb. Na. CEA.309/384/02/53 ya tarehe 10 Novemba, 2022 ili kupata ushauri wa kisheria kuhusu namna bora ya kushughulikia agizo hilo na hatimaye kuandaa taarifa ya utekelezaji.

"Mkurugenzi wa Mashtaka aliunda Kamati Maalum yenye wajumbe saba ambayo ilifanya mapitio kwa kufanya uchunguzi upya na hatimaye kubaini shauri hili haliwezi kurudishwa tena mahamakani kutokana na kukosekana ushahidi wa kutosha kuthibitisha shauri hili mahakamani dhidi ya watuhumiwa na hatimaye kuwatia watuhumiwa hatiani," alisema.

Alibainisha kamati hiyo ilishauri Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ichukue hatua za kinidhamu dhidi ya wahusika kwa namna kila mmoja alivyoshiriki ambapo watumishi 30 wamepewa barua ya onyo Aprili 24, 2023 na watumishi wawili wamepewa adhabu ya kutopandishwa cheo kwa muda wa miaka mitatu.

Kutokana na hatua hiyo, Kaboyoka alisema kamati ina maoni kuwa hatua zilizochukuliwa sio toshelevu kwa kuwa ukaguzi ulithibitisha kuwa watendaji husika walitenda makosa ya jinai ikiwa ni pamoja na kuingilia mfumo wa visa mtandao na kuiba fedha hizo.

**DART, KARIAKOO**

Kaboyoka alisema Bunge liliazimia ufanyike ukaguzi wa kiuchunguzi wa Shirika la Masoko Kariakoo ili kubaini iwapo kuna ubadhirifu wa fedha za umma uliofanyika na kufichwa baada ya soko hilo kuungua moto.

Alikumbusha kuwa kwa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), Bunge liliazimia CAG kufanya ukaguzi maalum wa malipo ya fidia Sh. bilioni moja na malipo ya fedha za usumbufu Sh. milioni 434 yaliyofanyika DART ili kubaini iwapo yalifanyika kwa mujibu wa sheria.

"Uchambuzi wa taarifa ya uhakiki ya CAG kwa Shirika la Masoko Kariakoo umebaini CAG amekamilisha mpangokazi kwa ajili ya ukaguzi maalum wa shirika hilo na umepelekwa kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - TAMISEMI pamoja na hati ya madai mnamo tarehe 31 Machi 2023 kwa ajili ya uwezeshwaji wa timu ya ukaguzi ili ukaguzi huu ufanyike. Hivyo azimio hili lipo katika hatua za utekelezaji," alisema.

Kwa DART, Kaboyoka alisema taarifa ya uhakiki ya CAG imebainisha kuwa ukaguzi maalum ulianza Mei 15, 2023 na unategemea kukamilika mwishoni mwa mwezi huu, yaani kesho na hivyo azimio hilo lipo katika hatua za utekelezaji.

**TUZO NA TOZO**

Mwenyekiti huyo alisema katika ukaguzi wa Mfuko wa Tuzo na Tozo wa Jeshi la Polisi, kamati imejipanga kupitia na kuchambua taarifa ya ukaguzi huo maalum mwezi Agosti, 2023 na kisha kuwasilisha taarifa yake bungeni.

"Mfuko wa Tuzo na Tozo wa Jeshi la Polisi, ukaguzi maalum ulikamilika. Kuhusiana na Mlipaji Mkuu wa Serikali kuandaa kanuni za kusimamia uendeshaji wa Mfuko wa Tozo na Tuzo mchakato huo unaendelea na sasa hatua ya kupata maoni ya wadau imekamilika na rasimu ya kanuni imewasilishwa kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani," alisema.

**UKAGUZI KADCO**

Kaboyoka alisema kamati ina maoni kuwa ukaguzi wa kina wa hesabu za Kampuni ya Uendelezaji wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KADCO) za mwaka 2010 hadi 2023 unaoendelea sasa, ukamilike kama ilivyopangwa na Bunge lichukue hatua stahiki zaidi kwa kuzingatia matokeo ya ukaguzi huo.

**TCB, TIB**

Mwenyekiti huyo alisema kamati inazitaka Benki ya Biashara Tanzania (TCB) na Benki ya Maendeleo (TIB) ziendelee kudhibiti ongezeko la mikopo chechefu na kuzingatia kikamilifu masharti ya Sheria ya Benki Kuu kuhusu ukwasi wa benki.

Alifafanua taarifa ya serikali imefafanuwa TIB, katika kipindi cha 31 Machi 2022 hadi 31 Machi 2023 imekusanya Sh. billioni 1.5 kutoka katika kundi la mikopo chechefu na kiwango cha mikopo chechefu kimefikia Sh. bilioni 77.95 Machi 2023 kutoka Sh. bilioni 357.90 kama ilivyokuwa kwa kipindi kilichoishia Machi 2022.

**BANDARI TANGA**

Kaboyoka alizungumzia ubadhirifu wa Sh. bilioni 64.3 katika upanuzi wa Bandari ya Tanga, akifafanua kuwa uchambuzi wa kamati katika taarifa ya serikali kuhusu azimio la kuchukua hatua kwa ubadhirifu wa fedha za umma, umebaini serikali imeliwasilisha suala hilo kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kwa ajili ya hatua za kisheria.

Alisema kamati inaona ni muda mrefu umepita bila hatua za kisheria kuchukuliwa kwa suala la ubadhirifu katika zabuni ya upanuzi wa Bandari ya Tanga.

"TAKUKURU wamepokea taarifa ya ukaguzi maalum kwa takribani miezi saba iliyopita, hivyo walitakiwa kuchukua hatua stahiki kwa wahusika," alisema.

**UDHIBITI WA NDANI**

Kaboyoka pia alisema kamati ina maoni kuwa hatua za ziada za kuwafikisha mahakamani watu wote waliohusika na ubadhirifu katika usimikaji wa mifumo katika Mamlaka ya Bandari (TPA) ziendelee kuchukuliwa.

Pia alisema kwa upande wa SUMA JKT, kamati ina maoni kuwa azimio la Bunge la kuwachukulia hatua watendaji waliohusika kuuza matrekta bila mikataba halijakamilika.

**HATUA NHIF**

Kaboyoka pia alisema kamati imepitia hatua kadhaa ambazo serikali imechukua katika kuimarisha mifumo ya udhibiti katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ili kuondoa tatizo la ubadhirifu.

Hata hivyo, alisema kamati ina maoni kuwa azimio hili halijakamilika kutokana na CAG kutopata uthibitisho wa kuchukuliwa hatua kwa wanataaluma 111 walioripotiwa katika mabaraza ya kitaaluma kwa kukiuka viapo vyao vya kazi, hivyo kuisababishia NHIF hasara.



"Aidha, hapakuwapo uthibitisho wa kusitishwa mikataba kwa vituo vilivyodanganya kutoa huduma na CAG hakupata uthibitisho wa makusanyo ya Sh. bilioni 22.5 katika mfuko wa NHIF kama ilivyowasilishwa katika taarifa ya serikali," alisema.

Alifafanua kuwa taarifa ya CAG ilibainisha dosari katika usimamizi na udhibiti wa taarifa muhimu za wanufaika wa huduma za NHIF na gharama za matibabu ambapo pamoja na mambo mengine, ilibainika utolewaji wa huduma za uzazi kwa upasuaji kwa wanaume 731.

Alisema ukaguzi ulibaini NHIF kukataa kulipa malipo ya Sh. bilioni 3.18 kwa hospitali za serikali zilizotoa huduma kutokana na kuwa na mfumo wenye upungufu wa utambuzi na usimamizi wa taarifa.

Mwenyekiti huyo alisema Bunge liliazimia serikali ifanye uchunguzi wa Idara ya Usimamizi na Udhibiti wa Huduma NHIF ili kubaini iwapo inatekeleza majukumu yake ipasavyo.

Bunge pia liliazimia uchunguzi ufanyike kubaini watoa huduma ambao wamekuwa wakiihujumu NHIF kwa kuongeza gharama za matibabu kwa njia za udanganyifu na kisha kuchukua hatua stahiki.

**TANESCO, TPDC**

Kaboyoka pia alisema kamati inatambua na imezingatia hatua za serikali za kubadili madeni ya Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC) na Shirika la Umeme (TANESCO) kuwa sehemu ya mitaji ya mashirika hayo.

Pia alisema katika Shirika la Madini (STAMICO), kamati haikuridhika na hatua ya STAMICO kutowasilisha kwa CAG utekelezaji wa azimio la Bunge.

**MALIPO YA RIBA**

Kaboyoko pia alisema katika eneo la riba zinazolipwa katika mikataba ya ujenzi kutokana na kuchelewa kwa malipo kwa makandarasi na washauri wa miradi, kamati inashauri:

"Kamati inaendelea kusisitiza umuhimu wa kufanyika uchunguzi wa kina katika eneo hili ili kuokoa fedha za umma ambazo zinaweza kutumika katika maeneo mengine yenye uhitaji na kuleta tija kwa Taifa,"alisema.

**NAKISI TRIL. 2.81/-**

Mwenyekiti huyo pia alisema katika azimio la Bunge kuhusu nakisi ya ukusanyaji wa mapato kupitia Mamlaka ya Mapato (TRA) Sh. trilioni 2.81, kamati inaona azimio halijakamilika utekelezaji wake kwa kuwa azimio lilitaka kukamilisha mchakato wa mapitio ya mfumo mzima wa kodi ili kuhakikisha mapato stahiki ya serikali yanakusanywa.

Vilevile, alisema kamati ina maoni kuwa azimio la kufanya uchunguzi wa sababu za kushindwa kufikia malengo ya makusanyo ya kodi kwa upungufu unaohusu dosari za kimaadili na weledi kwa baadhi ya watumishi wa TRA halijafanyiwa kazi hadi sasa kwa kuwa hali hiyo inakwaza dhima ya Bunge kuisimamia serikali ipasavyo.

**MIKOPO HESLB**

Alisema katika ukaguzi wa ufanisi katika Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), taarifa ya uhakiki ya CAG imebainisha utekelezaji wa ukaguzi wa HESLB ulianza rasmi Mei 16, 2023 na unatarajiwa kukamilika ifikapo Juni 30, 2023.

"Katika Bodi ya Mikopo, CAG ameanza kufanya ukaguzi wa kina kuhusu utaratibu wa utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu nchini," alisema.

**HIFADHI YA JAMII**

Kaboyoka alisema azimio la Bunge kuhusu mifuko ya hifadhi ya jamii halijatekelezwa kikamilifu pamoja na serikali kuchukua hatua mbalimbali kuhusu madeni ya mifuko ya hifadhi ya jamii. Haijaandaa mpango wa malipo ya mikopo ya mifuko hiyo kama Bunge lilivyoazimia.

Alifafanua kuwa uchambuzi wa taarifa ya CAG ulibainisha kupungua uwezo wa mfuko wa PSSSF kulipa mafao yake pamoja uwepo wa deni ambalo mifuko ya PSSSF na NSSF inadai kwa serikali takribani Sh. trilioni 1.5.

"Bunge liliazimia kwamba, serikali iwasilishe Bungeni mpango wa malipo ya mikopo ya mifuko ya hifadhi ya jamii kwa madeni yote ambayo mifuko inadai serikalini. Mpango huo wa malipo uwasilishwe bungeni kabla ya kukamilika mwaka wa fedha 2022/23,"alisema.

Bunge limeweka utaratibu mpya wa kuzipa nafasi kamati zake kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa maazimio ya Bunge.

HABARI KITAIFA

# Waziri Mkuu: Bandari isitugawe

**Na Jenifer Gilla,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka Watanzania wasiruhusu mgawanyiko wa aina yoyote wanapokuwa wanatoa maoni yao kuhusu makubaliano ya Serikali ya Tanzania na Dubai ya kuanzisha ushirikiano wa kiuchumi na wa kijamii katika uendeshaji wa maeneo ya bandari nchini.

Ili kujiepusha na hali hiyo, kiongozi huyo amewataka wananchi waepuke kujadili itikadi za kisasa, udini, ukabila, ukanda au vyovyote ili kuenzi tunu ya amani na mshikamano wa taifa iliyojengwa na waasisi wao.

Majaliwa alitoa kauli hiyo jana bungeni jijini hapa alipotoa hoja ya kuahirisha mkutano wa 11 wa Bunge la 12, akielekeza Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi iendelee kutoa elimu na ufafanuzi wa hoja za wananchi kuhusu makubaliano na mikataba ili utofauti wa hatua hizo mbili uwe wazi.

Alisema makubaliano ya mkataba huo yamekuwa na maoni mbalimbali kutoka kwa wabunge, wanazuoni na wananchi katika baadhi ya vipengele vya makubaliano ikiwamo umiliki wa bandari, muda wa mkataba, ajira za wazawa, ulinzi na usalama wa nchi na manufaa yatakayotokana na mikataba itakayoingiwa.

"Kwa upande mwingine, baadhi ya waheshimiwa wabunge na wananchi wameiomba serikali kuwa makini ili mikataba itakayoingiwa katika uendeshaji wa bandari iwe na tija kwa Taifa letu," alisema.

Majaliwa alisema makubaliano yaliyoingiwa yanalenga kuweka msingi wa ushirikiano baina ya serikali hizo mbili na maeneo ya uwekezaji, yatakayopendekezwa yataingiwa mkataba kwa kila eneo, hivyo masuala ya mfumo wa uwekezaji, mgawanyo wa mapato, muda wa uwekezaji na ukomo yatajadiliwa kwa kina.

Kuhusu umiliki wa bandari, Waziri Mkuu aliwahakikishia Watanzania kuwa kupitia Sheria ya Bandari ya Mwaka 2004, Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) imekasimiwa haki ya kuwa mmiliki wa maeneo yote ya bandari nchini na haina uwezo wa kutoa umiliki huo kwa kampuni yoyote.

Alisema wakati wote wa utekelezaji wa makubaliano hayo na mikataba itakayoingiwa, vyombo vya ulinzi na usalama vitaendelea kutekeleza majukumu yake katika eneo la mradi kama vilivyofanya katika kipindi cha miaka yote 22 ya mkataba na mwekezaji wa awali (TICTS) aliyemaliza mkataba wake mwezi Novemba 2022.

"Kuhusu mapato, ninapenda kuwahakikishia Watanzania kuwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) itaendelea kusimamia masuala ya mapato ya serikali kutoka kwa mwekezaji kwa mujibu wa sheria na mkataba," alifafanua.

Majaliwa alisema serikali iliamua kutafuta kampuni yenye uwezo na uzoefu mkubwa katika uendeshaji wa bandari duniani kwa teknolojia za kisasa ili kuiwezesha kufanya kazi kwa ufanisi, kuongeza mapato ya nchi, ajira na kuchagiza sekta nyingine za kiuchumi.

Alisema ushirikiano huo utatatua changamoto mbalimbali katika bandari hiyo ikiwamo kupunguza msongamano wa meli baharini, kupunguza muda mwingi unaotumika kupakua na kutoa mizigo bandarini ambao huleta athari mbalimbali.

Alisema ushirikiano huo pia utapunguza gharama za bidhaa kwa walaji na baadhi ya wafanyabiashara kutoka nchi jirani kukwepa kutumia bandari za nchini humo na kusababisha serikali kupoteza mapato ambayo yangetumika kutekeleza miradi ya maendeleo.

Aliwaomba wabunge na wananchi kuendelea kuiunga mkono serikali na kutambua alichokiita dhamira njema ya kuwaletea maendeleo.



Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, SACP Jumanne Muliro, akionyesha kwa waandishi wa habari jana, viroba vya bangi na vitu mbalimbali vya wizi vilivyokamatwa katika operesheni. P**ICHA: JUMANNE JUMA**

# ...aagiza mikutano ya serikali ifanyike kwa njia ya mtandao

**Na Jenifer Gilla,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amezielekeza wizara na taasisi za serikali zifanye vikao kwa njia ya mtandao kila inapowezekana ili kupunguza matumizi makubwa ya fedha za umma na gharama zisizo za lazima za uendeshaji wa vikao hivyo.

Vilevile, amewaelekeza maofisa masuhuli waimarishe usimamizi wa matumizi ya fedha za umma na kutekeleza kikamilifu Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2023/24.

Katika hotuba yake ya kuahirisha mkutano wa 11 wa Bunge la 12 bungeni jijini hapa jana, Waziri Mkuu alielekeza vikao vya kiserikali vifanyike kwa njia ya mtandao kwa kadri inapowezekana, ili kubana matumizi fedha za umma na kuepusha gharama zisizo za lazima za uendeshaji wa vikao hivyo.

Majaliwa pia aliwaagiza watendaji wa serikali kuzingatia kanuni, sheria na taratibu katika ununuzi wa umma ili kufikia shabaha na malengo ya uchumi, kuimarisha ukusanyaji wa mapato na kufanya matumizi kwa kuzingatia maeneo ya vipaumbele kwa mwaka huo.

Waziri Mkuu alielekeza taasisi za serikali kukamilisha malipo ya huduma na malimbikizo ya tozo na michango ya mifuko ya hifadhi ya jamii, kusimamia uhifadhi wa mazao ya chakula, kuboresha mifugo na kutatua migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

Mengine aliyoelekeza ni uhifadhi wa mazingira na upatikanaji wa maji, upangaji miji na utatuzi wa migogoro ya umiliki wa viwanja.

Kuhusu ukamilishaji wa malipo katika mifuko ya jamii, Majaliwa alizielekeza taasisi za serikali kukamilisha malimbikizo ya tozo na michango katika mifuko hiyo ifikapo Septemba 30, mwaka huu ili kuwaondolea usumbufu watumishi pindi wanapostaafu.

Alisema baadhi ya waajiri wamekuwa hawatunzi kumbukumbu za michango ya waajiriwa na kutowasilisha kwa wakati michango na tozo za watumishi katika mifuko hiyo, hivyo kusababisha usumbufu kwa watumishi pindi wanapostaafu.

"Ninazielekeza taasisi zote za serikali kulipia huduma wanazopata kutoka taasisi nyingine ikiwamo Shirika la Umeme (TANESCO), Shirika la Mawasiliano (TTCL), Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Wakala wa Majengo (TBA) na mamlaka za maji ifikapo tarehe Septemba 30, 2023 ili kuepusha kukwamisha uendeshaji wa taasisi hizo," aliagiza.

Kuhusu usimamizi wa mazao ya chakula, Waziri Mkuu alisema serikali imetenga Sh. bilioni 320 kwa ajili ya ununuzi wa nafaka kupitia Wakala wa Hifadhi ya Taifa ya Chakula (NFRA) na kumwelekeza Waziri wa Kilimo, Husein Bashe kusimamia utekelezaji huo ili ufanyike kwa wakati na kwa ufanisi.

Alisema serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya kuhifadhia chakula kwa ajili ya kuimarisha hali ya usalama na upatikanaji wa chakula nchini na kutoa kipaumbele cha ujenzi wa maghala.

"Vilevile, nitumie fursa hii kuwakumbusha wananchi umuhimu wa kuhifadhi chakula katika ngazi ya kaya na kuepuka matumizi ya chakula yasiyo sahihi," alisema.

Waziri Mkuu pia alielekeza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Wizara ya Mifugo na Uvuvi zishirikiane kubainisha na kutenga maeneo kwa ajili ya shughuli za ufugaji wakati wa utekelezaji wa miradi ya upangaji miji na vijiji.

Pia alilielekeza Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), lifanye tathmini ya uharibifu wa mazingira nchini na kuweka mikakati itakayowezesha shughuli za kilimo, umwagiliaji na ufugaji kufanyika bila kuharibu vyanzo vya maji na maeneo yaliyohifadhiwa.

Alizitaka mamlaka za mabonde zisimamie kikamilifu vibali vya matumizi ya maji kwa kuzingatia mahitaji ya watumiaji wengine na uendelevu wa upatikanaji wa maji katika maeneo husika na kuelimisha wananchi kuhifadhi vyanzo vya maji na maeneo yaliyohifadhiwa.

## Polisi yanasa 48 tuhuma uhalifu

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam limewakamata watu 48 wakiwamo watano wanaohojiwa kwa tuhuma za kupokea mali za wizi kutoka kwa wahalifu na kuzifanya sehemu ya biashara zao.

Kamanda wa Kanda hiyo, Jumanne Muliro, aliwaambia waandishi wa habari jijini hapa jana kuwa watuhumiwa hao wamekamatwa kupitia operesheni maalum iliyoanza mwezi Aprili mwaka huu.

Alisema miongoni mwa watuhumiwa hao wanadaiwa kujihusisha na matukio ya unyang'anyi na uvunjaji nyumba usiku na kuiba.

"Katika jitihada za kuzuia na kupambana na dawa za kulevya, Jeshi la Polisi limemkamata muuzaji sugu wa bangi Maneno Mayoge, maarufu Bundala (28), mkazi wa Majimatitu, Mbagala, Temeke.

"Amekamatwa na wenzake wawili wakiwa na bangi magunia saba, puli 445, mbegu za bangi kilogramu tano na magazeti ya kufungia bangi wakiwa wamejificha katika nyumba yao," alidai.

Pia alisema Jeshi la Polisi limewakamata watuhumiwa watatu wanaodaiwa kujihusisha na uporaji wa mikoba kwa kutumia pikipiki.

Kamanda Muliro pia alisema wamekamata pikipiki namba MC 252 DTG aina ya Boxer, akisisitiza Jeshi la Polisi limejipanga kuimarisha ulinzi na usalama wakati wa sikukuu ya Eid Alhaj.

# Eneo Gerezani kuwa la kimataifa

**Na Joseph Mwendapole**

WAKALA wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) imewataka wawekezaji kuwa tayari kwa ajili ya kulifanya eneo la Gerezani Kariakoo kuwa la kimataifa kwa kuwekeza kwenye hoteli za kisasa, maduka makubwa, ofisi na maeneo ya kupumzika.

Mtendaji Mkuu wa DART, Dk. Edwin Mhede, alisema hayo jijini Dar es Salaam wakati wa kikao kazi baina ya wakala na maofisa wa Shirika la Maendeleo la Japan (JICA) na taasisi mbalimbali nchini.

Alisema wanataka kuigeuza Gerezani kuwa eneo la kisasa kutokana na umuhimu wake wa kuunganisha awamu nne za mradi wa BRT na kuwa ni makutano ya mamilioni ya watu siku zijazo.

"Watu watakaotoka nchi za nje wataingia kwenye mfumo wa BRT mpaka Gerezani, msafiri akitoka upande wowote wa nchi atakuwa na uwezo wa kufika Gerezani kwa mfumo wa BRT sasa tutaweka miundombinu ya kutosha kuhakikisha mtu akitaka maduka anayakuta pale, hoteli, ofisi za kisasa na maeneo ya wazi kwa ajili ya mazungumzo," alisema Mhede.

"Tunaendelea kujipanga ndiyo maana tuko kwenye vikao kama hivi na wadau mbalimbali wa maendeleo kama JICA na tukiwa tayari tutawatangazia wawekezaji ili tuendeleze lile eneo kwa miradi ya ubia," alisema Dk. Mhede.

Alisema hata wakati wa msimu wa Sabasaba, Gerezani kunakuwa na watu wengi na wameshaona kwamba kwa sasa eneo hilo linaanza kuwa dogo kulinganisha na mahitaji na idadi kubwa ya watu.

"Tumejifunza kwa wenzetu waliofanikiwa kuweka uwekezaji kwenye shoroba za BRT kama Singapore na London - Uingereza, tunafanyakazi hii kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali za umma ndiyo maana hapa unawaona wawakilishi wa mamlaka mbalimbali," alisema Dk. Mhede.

Alisema watafanikisha azma hiyo kwa kushirikiana na Wakala wa Barabara za Nchini (Tanroad), Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Halmashauri na Manispaa za Jiji la Dar es Salaam kwa kuwa kuna maeneo watalazimika kutwaa ardhi kwa ajili hiyo.

Alisema kwenye shoroba ambazo mabasi ya BRT yatapita, watatwaa ardhi ambayo itatoa fursa za uwekezaji kwenye huduma kama za majengo ya maduka, kumbi za mikutano na ofisi na hata makazi nafuu na maeneo ya wazi.

"Wakati tunafanya usanifu wa mradi huu mwaka 2005 lengo lilikuwa ni kuondoa msongamano wa watu, lakini hatukuwa tumejielekeza kwenye kuendeleza shoroba zetu, lakini baadaye tukaona kuna sababu ya kuwekeza kwenye shoroba ndiyo maana tunataka kuifanya Gerezani iwe ya kimataifa na huduma zote muhimu zipatikane pale," alisema.

Alisema duniani kote miradi ya usafiri wa umma haiishii kusafirisha watu pekee bali inaambatana na uwekezaji mkubwa kwenye shoroba zake ambazo mabasi hayo yanapita ili kuwawezesha abiria kupata huduma mbalimbali kwa wakati na sehemu moja.

Alisema JICA wanatoa elimu ya namna ya kutekeleza uwekezaji kwenye shoroba na wanashirikiana na DART na taasisi mbalimbali za serikali kutengeneza mpango mkakati wa utekelezaji wa miradi hiyo.

"JICA wanatusaidia kutengeneza miongozo ambayo itaakisi mazingira yetu kwa kutumia uzoefu wa kimataifa ili kulifanya Jiji letu kuwa nadhifu zaidi na lifanane na majiji mengine yaliyoendelea kwingineko duniani," alisema Dk. Mhede.

ARA Hitoshi, ambaye ni Mwakilishi wa JICA nchini, alisema shirika hilo limekuwa likiisaidia Serikali ya Tanzania katika miradi ya kupanga mifumo ya usafiri na ujenzi wa miundombinu kama uboreshaji wa barabara ya Bagamoyo, daraja la Gerezani, daraja la Mfugale Tazara na mengineyo.

"Sisi Japan tuna uzoefu mkubwa sana wa uendelezaji miradi kwenye shoroba za BRT na tutafurahi kuona Watanzania wanatumia fursa hii kama sehemu ya kuboresha miji yao kwa kuwekeza kwenye biashara mbalimbali. Mipango miji ni jambo muhimu sana na usimamizi wake unapaswa kuwa makini sana," alisema Hitoshi.



Huzaifa Saifuddin (kulia), akishiriki kuchuna mbuzi katika maeneo ya Kisutu jijini Dar es Salaam jana, ikiwa ni maadhimisho ya Sikukuu ya Eid al-Adha. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# 'Serikali haijayatekeleza maazimio ripoti ya CAG'

**Na Jenifer Gilla,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) imeeleza kusikitishwa na kutotekelezwa kikamilifu maazimio 12 ya Bunge, ikiutaja ni uzembe wa makusudi uliofanywa na baadhi ya maofisa masuhuli katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Halima Mdee, aliyasema hayo juzi bungeni alipowasilisha taarifa ya utekelezaji wa maazimio ya Bunge yaliyotokana na ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuhusu ukaguzi wa hesabu za serikali za mitaa kwa mwaka 2020/21.

Mdee alisema uzembe wa kutotekeleza maazimio uliofanywa na maofisa hao unaashiria Mamlaka za Serikali za mitaa kulidharau Bunge.

Alisema kati ya maazimio hayo hayo, matano hayajatekelezwa kabisa, likiwamo la upatikanaji wa ruzuku ya maendeleo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mengine ni kuhusu uwekezaji wa mitaji ya umma, ununuzi na mikataba ya utoaji wa huduma na bidhaa, stahiki za watumishi kwa mujibu wa sheria na upotevu wa mapato katika mifumo ya kieletroniki ya kukusanya mapato.

Pia kulikuwa na azimio kuhusu utoaji wa mikopo ya makundi maalum ambapo halmashauri 155 zilishindwa kukusanya Sh. bilioni 47.01. Imetekelezwa kwa asilimia 34.

Kuhusu azimio la kuchukua hatua kali za kisheria dhidi ya watendaji wote wanaokusanya mapato nje ya utaratibu, Mdee alisema halijatekelezwa kabisa.

Alibainisha kuwa taarifa ya mwaka 2021/22 inanyesha kuwa katika mwaka wa fedha 2020/2021 kulikuwa na jumla ya mapendekezo yasiyotekelezwa 10,625. Kati yake, 4,408 (asilimia 42) yametekelezwa.

Kwa mujibu wa Mdee, hakuna utaratibu maalum kwa ajili ya utekelezaji wa maazimio ya Bunge baina ya taasisi za serikali na kusababisha vielelezo muhimu kushindwa kufikishwa kwa CAG kwa wakati kwa ajili ya uhakiki, jambo ambalo ni kinyume cha Ibara ya 143(3) ya Katiba ya Tanzania na Kifungu cha 11(a) na (b) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Sura ya 418.

"Serikali iliwasilisha taarifa ya utekelezaji tarehe 25 Mei 2023 na siku nne baadaye tarehe 29 Mei 2023 ndipo ilipowasilisha baadhi ya vielelezo, hali iliyopelekea CAG kushindwa kufanya jukumu lake la uhakiki wa majibu ya serikali kikamilifu," alisema Mdee.

## Aliyeshtakiwa tuhuma kuua mchungaji ahukumiwa kunyongwa hadi kufa

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

HATIMAYE aliyeshtakiwa kwa kumuua mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Iringa, amehukumiwa kunyongwa hadi kufa na Mahakama ya Hakimu Mkazi Iringa (yenye mamlaka ya nyongeza).

Mshtakiwa huyo Naftari Lulandala (20), alihukumiwa kifungo cha kunyongwa hadi kufa baada ya kukutwa na hatia ya kumuua aliyekuwa mchungaji wa KKKT Dayosisi ya Iringa, Elizabeth Ng'unga.

Akisoma Hukumu hiyo, Hakimu Mkazi Mkuu, Said Ally Mkasiwa, alisema kutokana na ushahidi uliotolewa Naftari alitenda kosa hilo la kumnyonga mchungaji Elizabeth na alikuwa mtu wa mwisho kuwa naye.

Ilidaiwa Naftari alimnyonga mchungaji Elizabeth kwa kamba ya manila iliyokuwa na rangi ya njano kisha mwili wake kuutupa vichakani.

Lulandala ilidaiwa alitenda kosa hilo Desemba 10, mwaka 2021 katika Kijiji cha Kipaduka na mchungaji Elizabeth alikwenda kwa ajili ya kufanya biashara ya mahindi.

Siku ya tukio mtuhumiwa alimuaga mke wake kwamba anakwenda kumchukua mchungaji Elizabeth ambaye ni shemeji yake ili ampeleke shambani kwa kutumia pikipiki yake kwa sababu alikuwa amepewa shilingi milioni tatu kwa ajili ya kufanya biashara ya mahindi, badala yake alirudi nyumbani akiwa na begi la marehemu na kumwambia mkewe kuwa dada yake atarudi baadaye.

Hata hivyo, mke wake alisikia habari za kuuawa kwa mtu katika mashamba na alipomuuliza mumewe alisema hata yeye amesikia, lakini pikipiki yake haina mafuta na kudai hawezi kwenda kutazama.

Kesi hiyo ilikuwa na mashahidi kumi akiwamo daktari aliyethibitisha kuwa Elizabeth alinyongwa kutokana na alama za shingoni na alikufa kutokana na kushindwa kupumua.

Shahidi mwingine ni mdogo wa marehemu ambaye ni mke wa mshtakiwa ambaye aliiambia mahakama kuwa siku ya tukio mumewe alimuaga anakwenda kuchumchukua dada yake ili waende shambani kwa pikipiki yake badala yake alirudi na begi lake dada yake bila kuwa naye.

Aaron Mkumbo ambaye ni mume wa marehemu alipoona mkewe hapatikani kwenye simu kwa siku mbili aliamua kwenda kutoa taarifa katika kituo cha polisi na taratibu za kuanza kumtafuta zikaanza kufanyika.

Baada ya siku tano kupita, Mkumbo alisikia taarifa za kuuawa kwa mwanamke ambaye hakujulikana jina na alipopelekwa Hospitali ya Ilula na kuonekana hana ndugu hospitali iliamua kumzika kwa sababu alikuwa na majeraha.

Taratibu za kwenda kuufukua mwili huo zilifanyika na kwenda kuzikwa upya siku hiyo hiyo kwa kuwa mwili ulikuwa umeanza kuharibika.

Kesi hiyo imeendeshwa na mawakili wa serikali Margret Mahindi na Sophia Mwanjoti, ambao waliiomba mahakama kutoa adhabu kali kama sheria inavyoelekeza kutokana na kitendo hicho cha kikatili kufanywa na mtuhumiwa.

## Chongolo aonya UVCCM kutanguliza maslahi binafsi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, ameuonya Umoja wa Vijana wa chama hicho (UVCCM) dhidi ya kukubali kuwa sehemu ya kubeba maslahi binafsi ya watu wachache.

Chongolo alitoa onyo hilo juzi jijini hapa alipohutubia wajumbe wa Baraza Kuu la umoja huo, akisema CCM inategemea vijana hao kutumia nafasi zao kubeba agenda za chama zenye maslahi kwa taifa na watanzania.

Aliwataka wasikubali kuwa sehemu ya kubeba maslahi binafsi ya watu wachache wenye ndoto zinazokinzana na misingi ya chama.

"Chama chetu kinawategemea sana jumuiya hii kukilinda na kukisemea na kufanya mambo yakayokifanya kiendelee kuwa chama tawala nchini na si vinginevyo, tusiache wajibu huo, tusiache kulinda viongozi wetu, tusibebe jukumu la kuwa viongozi wa watu," alionya.

Aliongeza "...hasara ya kuwa kiongozi wa mtu ni hasara unayojitengenezea kuwa daraja la kukuharibia kesho yako. Ukiwa kiongozi unayesimama na kujitegemea, utaishi miaka yote ukiwa unaendelea kufaidi fursa ya uongozi uliojitengenezea mwenyewe.

"Lakini ukiamua kuwa kiongozi mfuasi wa mtu, yule mtu akiondoka, na wewe unakwenda na maji. Na mara nyingi watu tunao wafuasi ni ambao watu wenye ndoto.

"Kuna watu maisha yao ni ndoto na ni ndoto kwelikweli. Acheni na achaneni na ndoto za watu. Ishi na ndoto za uhakika, ndoto za taasisi... ndoto za CCM.

"Simameni na viongozi halali na sahihi wa taasisi na sio viongozi wanaojiandaa kuwa viongozi bila kuandaliwa na taasisi. Viongozi wengi wanaojiandaa na kuwa na tamaa ya nafasi, kwenye chama hiki huwa hawapati nafasi. Nendeni kwenye historia. Sasa ninyi msiwe wafuasi wa wanaojiandaa. Kuweni wafuasi wa taasisi."

Mwenyekiti wa UVCCM Taifa, Mohamed Ali Mohamed, alisema "...nitoe wito na kwenu na ninyi mnavyo vikao vyenu kule chini, kwa wenyeviti, makatibu pamoja na wajumbe wa Baraza Kuu.

"Niwaombeni sana mkasimamie vikao hivyo, viendelee na vifanyike. Kwa sababu kwenye vikao ndipo tunapotoka na maazimio yote ya pamoja, kauli ya pamoja na uelewa wa pamoja.

"Lakini sambamba na hilo, niwekee mkazo katika suala zima la ziara. Niwapongeze baadhi ya maeneo, nimekuwa nikiwafuatilieni kwa karibu.

"Mmekuwa mkifanya ziara katika maeneo yenu. Niwaombe kwa wale bado. Ziara hizo zikaanze au zikaendelee. Na ziara hizo zikianza ama zikiendelea, basi zisiwe ziara za kupiga picha, bali ziwe ziara za kuleta tija katika chama chetu na kwa Mwenyekiti wetu wa Chama Cha Mapinduzi," alisema.




Daladala yenye namba za usajili T 326 DXC inayofanya safari zake kati ya Kigogo Sokoni na Simu2000 limegongana na bajaji ya kubeba mizigo, eneo la Ukonga-Magereza jijini Dar es Salaam jana. Dereva wa bajaji amepata majeraha mguuni. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Serikali yataja maeneo saba uboreshaji Bandari

**Na Restuta James**

SERIKALI imetaja maeneo saba ya haraka ambayo yataboreshwa iwapo Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) na kampuni ya DP World, zitafanikiwa kuingia mikataba ya uwekezaji.

Aidha, imewashukuru wananchi na wadau kwa kutoa maoni, ambayo kwa sehemu kubwa yatazingatiwa kwenye majadiliano ya mikataba ya uwekezaji kati ya DP World na TPA.

Akizungumza na NIPASHE ofisini kwake jijini Dar es Salaam jana, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Uchukuzi), Dk. Ally Possi, alisema TPA itaendelea kuendesha gati 8-11, KOJ1, KOJ2 na SPM na kwamba haki ikiwamo ya kumiliki ardhi anayopewa mwekezaji huyo kupitia IGA, itasimamiwa na sheria za Tanzania.

Alitaja kuwa Bandari ya Dar es Salaam inauhitaji wa haraka wa vifaa vya kisasa vya kupakua na kupakia mizigo melini, mifumo ya teknolojia inayosomana, kuongeza ujuzi kwa watumishi na ongezeko la mapato na ushuru, kutokana na shehena itakayohudumiwa.

Alisema serikali inahitaji maboresho hayo ili kuiwezesha bandari hiyo kushindana na nyingine za jirani, kuongeza kodi na ushuru na kupata mtandao mkubwa wa biashara ya bandari duniani.

Dk. Possi alisema kwa mujibu wa makubaliano kati ya Tanzania na Dubai (IGA), maeneo ya uwekezaji yanayotajwa kwenye kiambatanisho namba moja ni uendelezaji na uendeshaji wa gati 0 (ya magari), 1-4 (mizigo mchanganyiko) na 5-7 (makasha), kuboresha magati la abiria na majahazi, ambayo yataendeshwa na TPA, kuendeleza, kusimamia na kuendesha bandari kavu ya Kwala na maeneo huru ya kiuchumi.

Dk. Possi ambaye amebobea katika sheria za kimataifa, alisema eneo lingine la uwekezaji ni kuendeleza, kusimamia na kuendesha kituo kipya cha kuhudumia magari na makasha, kufunga mifumo ya kisasa ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), kulingana na maelekezo ya TPA, kutoa huduma za kisasa za bandari na kutoa mafunzo ya kitalaamu kwa watumishi wa mamlaka hayo,

"Muunganiko wa huduma hizo zinazotolewa na DP World na uendeshaji wa bandari kwa namna ambavyo DP World amekuwa akitoa huduma katika maeneo mbalimbali duniani, umekuwa chachu kubwa ya ukuaji wa uchumi wa nchi hizo kwa sababu za ufanisi mkubwa unaopatikana wakati wa utoaji wa huduma zenye muunganiko wa kuanzia usafirishaji wa shehena majini na nchi kavu," alisema.

Dk. Possi alisema maboresho hayo yataongeza shehena ya mizigo itakayohudumiwa kutoka tani milioni 18.41 za mwaka 2021/22 hadi tani milioni 47.57 mwaka 2032/33.

Alisema serikali inatarajia kuwa ongezeko hilo la shehena ya mizigo itaongeza mapao ya kodi ya forodha kutoka Sh. trilioni 7.76 mwaka 2021/22 hadi Sh. trilioni 26.7 mwaka 2032/33.

Alisema bandari itakapofungwa mifumo hiyo ya kisasa, itapunguza muda wa meli kusubiri nangani kutoka siku 5 hadi saa 24, wakati muda wa kupakia na kupakua makasha utapungua hadi siku mbili kutoka siku 4.5 za sasa.

"Tunatamani kuwa na vifaa vya kisasa ambavyo vitaleta ufanisi, mifumo inayosomana na hawa (DP World), wamebobea. Lingine ni ujuzi kwa watu wetu, tutapata mapato ya kumkodisha (gati), ya kuhudumia shehena na gawio. Ongezeko la mapato ya serikali kupitia Mamlaka ya Mapato (TRA) na ninaamini ni mambo ambayo tunaweza kuyapata ndani ya muda mfupi baada ya uwekezaji," alisema.

Alisema ufanisi wa bandari utachagiza kwa kiwango kikubwa sekta ya biashara na usafirishaji, akigusia pia njia ya reli.

Dk. Possi alisema: "Reli na bandari vina mahusiano makubwa na ni chachu ya uchumi...reli yetu itakuwa haina maana kama hatusafirishi mizigo na bandari yetu itakuwa haina maana kama haitoi mizigo."

Aliongeza kuwa lengo ni kuhakikisha kwamba mizigo ya nje ya nchi ikiwamo Congo itafika nchini humo ndani ya siku saba.

Kuhusu haki ya kumiliki ardhi, alisema kwa sheria na Katiba ya Tanzania, wawekezaji wanamilikishwa kwa utaratibu maalumu na kwamba DP World ataufuata..

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tanzania ina utajiri wa vivutio vya utalii vitangazwe

**UTALII** ni sekta muhimu kwa uchumi wa taifa. Ni sekta inayokua kwa kasi zaidi na kuchangia Pato la Taifa kwa asilimia 17.5 na fedha za kigeni asilimia 25.

Sekta hiyo pia inatoa ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja milioni 1.5.

Umuhimu wa sekta hiyo unaonekana pale watalii wanapotoka kwenye nchi zao na kumiminika nchini kuja kujionea vivutio na kuliingizia taifa fedha za kigeni.

Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) ambayo inahusika katika suala la watalii jukumu lake kubwa ni kuhamasisha sekta hiyo ili iweze kupata watalii wengi zaidi.

Njia moja ya uhamasishaji ni kuwaomba wadau mbalimbali kushirikiana na serikali kutangaza vivutio vya utalii vya nchini ili kuongeza wigo wa watalii ili lengo la kufikia watalii milioni tano wanaoingia nchini lifikiwe.

Tanzania imebarikiwa kuwa na vivutio vingi vya utalii, kuanzia wanyama, mimea, wadudu, mambo ya asili, fukwe za bahari ambavyo vikitangazwa kwa bidii, watalii wengi watamiminika.

Faida iliyopo sasa ni dunia inakwenda kidijitali hivyo ni rahisi kwa watalii walio katika nchi mbalimbali duniani kuona na kufanya utaratibu wa kuja kuvitembelea.

Nchi nyingine zinatumia fursa hiyo kutangaza vivutio ambavyo hata hapatikani nchini mwao, lakini ujanja wanaotumia na kuwaingiza watalii kwao na kisha kuwavusha kwenye nchi yenye vivutio hivyo huku wakifaidika na fedha za watalii hao kuanzia kwenye hoteli wanazofikia, vyakula na bidhaa wanazonunua.

Hivi karibuni Meneja Masoko wa TTB, Nassoro Garamatatu, wakati akizungumzia maandalizi ya safari maalumu ya kupeleka wafanyabiashara nchini China inayoratibiwa na kampuni ya GNM Cargo ya kutangaza vivutio mbalimbali vilivyoko Tanzania, alisema bado fursa ziko wazi kwa ajili ya kuongeza watalii nchini na endapo serikali na wadau watashirikiana itasaidia kufikia lengo lililopangwa la kuongeza zaidi idadi ya watalii nchini.

Bodi hiyo imeonesha utayari wa kuwakaribisha wadau mbalimbali wenye nia nzuri ya kutangaza vivutio vya utalii ambayo pia itachangia kuongeza pato la taifa na kuunga mkono jitihada zinazofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan katika kuinua sekta ya utalii nchini.

TTB imekuwa na mikakati mbalimbali ya kutangaza utalii zaidi duniani ikiwamo wa utamaduni na ndiyo maana inatoa fursa kwa wadau kwenda nchini China ili wakatangaze vivutio vya Tanzania. Safari hii maalumu ya kitalii, itakuza zaidi mahusiano mazuri baina ya serikali za nchi hizi mbili, wadau na wananchi wao, hivyo ni eneo ambalo litaongeza fursa za kukuza utalii.

Wafanyabiashara ambao ni wadau wakubwa katika sekta ya utalii wametakiwa kuzingatia taratibu za kuwaingiza watalii kwa kuwa na vibali stahiki.

Tanzania na nchi nyingine za Afrika Mashariki, zimeamua kuandaa safari kwa wafanyabiashara Oktoba mwaka huu ili kwenda kujifunza fursa mbalimbali za utalii nchini China, kutangaza na kuhamasisha fursa za utalii za Tanzania.

Wachina wamekuwa wakiingia kwa ajili ya masuala mbalimbali, lakini bado idadi yao ni ndogo katika eneo la utalii, hivyo safari hiyo itaongeza zaidi hamasa kwao kuja kuona vivutio vilivyopo nchini.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kamwe usifanye makosa haya kwenye hatua, itikadi za kumiliki fedha zako

Na Halfani Chusi

**UKOSEFU** wa matumizi sahihi ya fedha ya mkopo yamekuwa sababu ya wengi wao kufilisiwa mali zao, kwa kushindwa kurejesha kwa wakati.

Wakati mwingine hupelekea hata watu kupelekana mahakamani, kupokwa mali, kudhalilishwa kwenye jamii na hata kupelekea kutokuwa na uhusiano mzuri kati ya mkopaji na mkopeshaji.

Pesa ndio kila kitu jamani, hivyo naamua nikunong'oneze kanuni pori 12 zinazoweza kukuweka kwenye njia moja ya matumizi salama ya nyenzo hiyo. Hebu fuatilia kwa umakini, nikiamini itakutoa uliko.

Kwanza: Usikope fedha ya riba ili uanzishe biashara, Usitegemee fedha ya mkopo kuanzisha biashara, kwamba upate faida kisha uirudishe na riba yake.

Pili, usitumie fedha ambayo bado haipo mikononi mwako, wala usije ukamuahidi mtu kumpa ilihali na wewe umeahidiwa mahali fulani, kama kuna mtu kakwambia, "fulani njoo kesho nikulipe deni lako" wewe usiende kukopa vitu kadhaa dukani au hata kumuahidi mtu mwingine kumpa ikiwa na wewe umeahidiwa, ni kosa unaweza kujiingiza kwenye matatizo.

Tatu, kama unataka kuhifadhi au kutunza fedha, kila unapoipata, usianze kuitumia kwanza kisha ukategemea kutunza kiasi kitakachosalia. Hivyo, basi, ukiipata tu, weka pembeni kiasi unachodhani kinafaa kutunzwa au kuhifadhiwa kisha tumia kiasi kilichobaki.

Nne, ukipata nafasi ya kuonana na mtu tajiri, kamwe usiombe fedha, omba maarifa ya kutengeneza kipato kama yeye, tena kwa mtaji mdogo, maarifa ndio mtaji wa kwanza, unaweza kupewa au kusaidiwa iwapo una mawazo mazuri ya kuzalisha fedha, baadhi husema, "omba ndoano, usiombe samaki".

Tano, usitunze mbegu badala ya kuipanda, watu wengi hufurahia wanapolipwa kisha wanaiweka benki au nyumbani bila kuiwekeza, wekeza ili uzalishe zaidi, usiogope kuingia hasara, kila aliyefanikiwa alipoteza kwanza kabla hajafanikiwa. Wengi walipoteza muda, fedha, afya na hata matumaini ya kufanikiwa, ila kwa uthubutu wao, mwisho wa siku walifanikiwa.

Sita, kamwe usimkopeshe mtu fedha ambayo unahisi hatorudisha, unapo mkopesha mtu huyo jiridhishe mwenyewe moyoni kuwa kama hatoweza kulipa basi deni lake halitoathiri urafiki wenu, ukihisi urafiki utaharibika mshauri aende benki.

Saba, usikubali kuwa shahidi, tena kwa kusaini kabisa ili umdhamini mtu ambaye huna uhakika kuwa atalipa kile unachomdhamini, kumbuka maana ya kumdhamini mtu kwamba utawajibika iwapo atashindwa kulipa.

Nane, epuka kutembea na pesa nyingi ambazo hata huna matumizi nazo wakati huo, unaweza kujikuta unafanya matumizi ambayo hayakuwa kwenye ratiba sababu ya ushawishi wa fedha ya mfukoni.

Ili kuepuka haya, tembea na kiasi ulichopanga kukitumia katika safari yako. Fedha nyingine itunze mahali pengine palipo salama.

Tisa, epuka kutunza pesa mahali pasipo sahihi maeneo kama kwenye soksi, sidiria, chini ya mto wa kulalia, chini ya begi, kwenye kopo au hata kwenye begi la safari, si maeneo salama.

Ni rahisi kusahau, kuibiwa au kupoteza, ni bora ukatunza kielektroniki; yaani benki kwenye simu, au kwenye pochi yenye kamba ngumu ya kuivaa mabegani au pochi ambayo inatosha kwenye mifuko imara na yenye vifungo kwenye nguo zako hasa uwapo safarini.

Kumi, usitumie pesa kwa kitu ambacho hakikuwa kwenye ratiba yako, jiulize kwanza kabla hujanunua, "Bila kitu hiki, maisha yataenda au lah? Ukiona maisha yataenda bila kitu hicho, acha kukinunua, tabasamu kisha ondoka.

Kumi na moja, matumizi yako ya pesa yasizidi pato lako, ukiona unamatumizi makubwa ya kuzidi pato lako, unapaswa kuwa bahili katika matumizi yako, fanya matumizi makubwa pale tu pato lako litakapo ongezeka. Hii itakuepushia kushindwa kufanya baadhi ya mambo ya msingi na kisha ukajikuta unaishia kwenye madeni makubwa.

Kumi na mbili, kama una ndoto kubwa hapo baadaye, labda kujenga nyumba, kununua gari, kununua kiwanja, simu nzuri hata pikipiki. Usikurupuke, kwa sasa eti tu sababu umekipata kwa bei ya punguzo.

Usichanganye kati ya mahitaji ya baadaye na ya sasa, fedha unayotumia kutimizia ndoto sasa itumie kwa mahitaji ya sasa, ndoto ibaki kuwa ndoto hii itakuepushia kuingia katika madeni.

**Simu: 0787879707**

HABARI KITAIFA

# Muswada wa sheria mpya viwanja vya ndege waja

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Ujenzi na Uchukuzi inatarajia mwezi Septemba mwaka huu kuwasilisha bungeni muswada wa sheria utakaoweka msingi wa viwanja vyote vya ndege nchini kuwa chini ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA).

Naibu Waziri wake, Atupele Mwakibete, alitangaza mpango huo jana bungeni alipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Mwanaisha Ulenge.

Mbunge huyo alisema kuwa mwaka jana Bunge liliazimia kampuni ya Uendelezaji na Uendeshaji wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KADCO) kuwa chini ya TAA na kuhoji lini serikali itafanya hivyo kutekeleza azimio hilo.

"Lini serikali itakamilisha mchakato wa sheria kuipa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kusimamia na kuendeleza viwanja vya ndege nchini?" alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Mwakibete alisema baada ya Bunge kuazimia KADCO kuwa chini ya TAA, hatua ambayo imefanywa serikali hadi sasa ni kuelekeza TAA kuandaa mapendekezo ya sheria na tayari imeshafika wizarani na kuboresha na kupeleka kwa Mwanasheria Mkuu ambaye tayari ameshatoa kibali na kwa sasa suala hilo liko ngazi ya makatibu wakuu.

"Itapelekwa kwenye Baraza la Mawaziri litakalofanyika mwezi Julai mwaka huu na matarajio ya wizara mwezi wa Septemba itawasilisha bungeni muswada wa sheria ambao utaweka msingi wa viwanja vyote vya ndege nchini kuwa chini ya TAA.

"Kwa sasa ilivyo kuna viwanja vipo chini ya TANAPA vingine vipo chini ya taasisi zingine za serikali, hivyo sheria hii itaweka msingi viwanja vyote vya serikali nchini viwe chini ya TAA," alisema.

Katika swali la msingi, mbunge huyo alihoji lini TAA itapewa rukhsa kukusanya na kutumia tozo ya abiria kuboresha viwanja vya ndege.

Akijibu swali hilo, Mwakibete alisema TAA imewekewa utaratibu wa kukusanya moja kwa moja ada za kutua na maegesho ya ndege, ada ya usalama, tozo za ukodishaji wa ofisi, karakana, majengo ya kuhifadhia mizigo, migahawa na maduka, tozo za maegesho ya magari na tozo za mabango.

Alisema Sheria ya Huduma za Viwanja vya Ndege Sura ya 365, inaipa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) jukumu la kukusanya tozo kwa abiria wanaosafiri kupitia viwanja vya ndege na kuwasilisha Hazina.

"Fedha zinazokusanywa na TRA kutoka kwa abiria na kuwasilishwa Hazina, zinatumika kuendeleza miundombinu ya viwanja vya ndege nchini na kulipa mishahara ya watumishi, matumizi ya uendeshaji wa TAA na kufanya matengenezo ya viwanja,"alisema.

Pia alisema serikali hutoa fedha kila mwaka kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya viwanja hivyo.



Mkurugenzi Mwendeshaji wa Shirika la East Central and Southern Africa Health Community (ECSA), Sibusiso Sibandze (kulia), akizungumza katika uzinduzi wa kanzidata ya kuhifadhi takwimu za mwenendo wa ugonjwa wa kifua kikuu ndani ya mataifa 16 ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), kupitia mradi wa kuzuia kifua kikuu migodini, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wagonjwa wanaochuja damu walivyoongezeka Mloganzila

**Na Romana Mallya**

IDADI ya wagonjwa wanaopatiwa huduma ya kuchuja damu Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) - Mloganzila, imeongezeka kwa asilimia 72 kutoka wagonjwa 91 katika miezi mitatu ya mwanzo ya mwaka jana hadi kufikia wagonjwa 157 kwa kipindi kama hicho mwaka huu.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Figo hospitalini huko, Immaculate Goima, alimwambia mwandishi jana kwamba ongezeko hilo linachangiwa na maboresho ya huduma zinazotolewa hospitalini huko.

Pia alisema uelewa wa dalili za magonjwa yasiyo ya kuambukiza miongoni mwa jamii umeongezeka, jambo ambalo limechangia wagonjwa kufika hospitali kwa ajili ya uchunguzi na kuanza matibabu mapema.

Dk. Goima alisema Mloganzila imekuwa na utaratibu wa kutoa elimu kwa jamii ya namna ya kukabiliana na magonjwa yasiyo ya kuambukiza na pale wanapohisi kuwa na dalili zake, huwashauri watu kufika hospitalini mapema kwa ajili ya matibabu.

"Mloganzila tuna wataalamu wenye ujuzi na weledi katika matibabu ya magonjwa mbalimbali ikiwamo magonjwa ya figo. Tunatoa huduma kwa saa 24 kila siku, watoa huduma wetu wana ari, morali na wanajali wagonjwa, pia wanatoa huduma muda wote," alisema.

Akizungumzia huduma za kupandikiza figo, Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Figo hospitalini huko, Gyunda Anthony alisema Mloganzila ilifanya upandikizaji wa figo kwa wagonjwa watatu ambao wanaendelea vizuri pamoja na wale waliowachangia.

"Walipandikizwa figo Aprili mwaka huu, wanakuja kliniki kwa ufuatiliaji wa afya zao mara moja kwa mwezi. Kabla ya kupandikizwa figo walikuwa wanasafisha damu mara tatu kwa kwa wiki na kukaa zaidi ya saa nne kwenye mashine ya kuchuja damu kila walipohudhuria hospitalini kwa ajili ya huduma hiyo," alisema.

Bingwa huyo alitaja sifa za mgonjwa anayestahili kupandikizwa figo kuwa ni yule mwenye tatizo sugu la figo, umri chini ya miaka 60, asiwe na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (VVU) na homa ya ini, awe na akili timamu na uwezo wa kupata dawa za kushusha kinga baada ya upandikizaji.

Kwa anayechangia, daktari huyo alisema anatakiwa kuwa mwenye umri kati ya miaka 25 hadi 60, awe na afya njema ya akili, asiwe na maambukizi ya VVU na homa ya ini, asiwe na ugonjwa wa kisukari wala shinikizo la juu la damu.

Dk. Gyunda aliishauri jamii kufuata ushauri unaotolewa na wataalamu wa afya ikiwamo kufanya mazoezi, kuzingatia ulaji sahihi kwa kupunguza matumizi ya vyakula vya wanga na sukari na pia kula matunda na mboga mboga kwa wingi ili kuepuka kupata magonjwa yasiyoambukiza.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# PIC yaonyesha kutoridhishwa utekelezaji maazimio ya Bunge

**Na Jenifer Gilla,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) imeonyesha kutoridhishwa na utekelezaji wa maazimio saba kati ya 13 ya Bunge.

Maazimio ambayo hayajatekelezwa kikamilifu ni pamoja na upungufu wa mtaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) unaosababishwa na utaratibu wa kukodi ndege kutoka kwa Wakala wa Ndege za Serikali (TGFA).

Mengine ni taasisi kutokuwa na bodi za wakurugenzi kwa muda mrefu kutokana na kuchelewa kuteuliwa kwa wajumbe wa bodi, kutoiwezesha Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) na kuathirika kwa kilimo cha pamba kutokana na maelekezo ya serikali ya mwaka 2019 ya kuuza pamba kwa bei ya juu zaidi ya bei ya soko la dunia, jambo lililosababisha deni la Sh. bilioni 21.8 kwa serikali.

Mengine ni azimio la matumizi ya TEHAMA katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na matumizi makubwa ya gharama za bima za ndege kwa ATCL.

Mwenyekiti wa PIC, Jerry Silaa, alibainisha dosari hiyo wakati akiwasilisha bungeni juzi maoni ya kamati hiyo kuhusu utekelezaji wa maazimio 13 ya Bunge yaliyotolewa wakati wa kujadili taarifa ya kamati mwezi Novemba 2022.

Kuhusu ATCL, Silaa alisema Azimio la Bunge lilikuwa TGFA ikamilishe taratibu ya kurudisha ndege kwa kampuni hiyo kwa kuwa ukiondoa tatizo hilo, kampuni ina uwezo wa kujiendesha kwa faida.

Alisema uchambuzi wa kamati ulibaini serikali iliunda kamati ya pamoja ya kushughulikia jambo hili ikiwamo masuala ya kiufundi, kisheria na kimkataba na imekamilika na kuwasilishwa ripoti kwa Baraza la Mawaziri.

Kuhusu azimio la taasisi kutokuwa na bodi ya wakurugenzi kwa muda mrefu. Silaa alisema uchambuzi wa kamati umebaini kuna ucheleweshaji katika kupata bodi za wakurugenzi za mashirika ambapo Bunge liliazimia serikali itumie miezi mitatu kukamilisha uteuzi wa wajumbe wa bodi 12 katika taasisi ambazo tayari zina wenyeviti,

Alisema kuwa hadi kufikia tarehe ya kikao cha kamati, kati ya taasisi 12, saba ndizo zilikuwa zimekamilisha utekelezaji huo licha ya kutumia miezi saba tofauti na miezi mitatu iliyotolewa na Bunge.

Alisema Bunge pia liliazimia serikali itumie miezi sita kukamilisha uteuzi wa wajumbe wa bodi 23 katika wizara 12 ambazo hazina lakini hadi kufikia tarehe ya kuwasilisha taarifa hiyo ni taasisi 17 tu zilkuwa zimepatiwa bodi.

Kuhusu hatua za majadiliano katika mradi wa Mchuchuma na Liganga kuchukua muda mrefu, mwenyekiti huyo alisema kamati inasisitiza majadiliano kati ya Serikali na GNT yaendelee kwa umakini na yafike mwisho kwa kuwa bado hayafikia mwisho licha ya Bunge kuazimia yachukue miezi mitatu.

Kuhusu kuiwezesha TADB, Silaa alisema uchambuzi wa kamati ulibaini azimio hilo linatekelezwa japo sio kwa njia iliyokusudiwa awali ya kutoa Sh. bilioni 100 kila mwaka.

Kufuatia hali hiyo, Silaa alisema kamati inasisitiza serikali irejee katika ahadi yake kuipatia TADB kiasi hicho cha fedha kama ilivyoahidi kwa kuwa kama ingekuwa imetekelezwa, benki ingekuwa na mtaji wa Sh. bilioni 760, hivyo kuwa katika nafasi ya kutoa huduma kwa wakulima wengi zaidi.

Kuhusu kuathirika kwa kilimo cha pamba, kiongozi huyo wa kamati alisema Bunge liliazimia serikali iharakishe utekelezaji wa ahadi yake ya kulipa deni la pamba na uchunguzi wa kamati ulibaini serikali imekwishakamilisha uhakiki wa deni hilo lakini wakulima wahajalipwa fedha hizo.

Alisema kamati inasisitiza serikali itimize ahadi yake ya kulipa deni hilo ndani ya mwaka wa fedha 2023/24 na bajeti yake ionekane katika bajeti ya serikali ya mwaka huo.

Alisema maelekezo ya serikali ya mwaka 2019 ya kuuza pamba kwa bei ya juu zaidi ya bei ya soko la dunia yaliisababisha deni la Sh. bilioni 21.8 na kuathiri taswira ya Bodi ya Pamba kwa wakulima na kuongeza changamoto katika biashara hiyo.

Vilevile, alisema kuwa uchambuzi wa kamati umebaini kuwa pamoja na serikali kuripoti kuwa NHIF ina mifumo madhubuti ya TEHAMA, bado kuna malalamiko makubwa ya utendaji wa shirika hilo, hivyo wanaishauri serikali iandae mkakati madhubuti wa kulisimamia kwa kuwa kwa mujibu wa taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), shirika hilo haliko katika hali nzuri.



Diwani wa Kata ya Makumbusho, Dar es Salaam, Mohamed Ally akizungumza katika maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika iliyoandaliwa na shirika la Wanawake katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), kwa kushirikiana na Jumuiya ya Wazazi CCM kata hiyo, kwa ufadhili wa Woman Fund Tanzania (WFT) juzi, ikiwa ni sehemu ya kampeni ya kupinga rushwa ya ngono iitwayo 'Safari Salama Bila Rushwa ya Ngono Inawezekana'. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Maboresho mwongozo wa biashara ya kaboni yaiva

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SERIKALI kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais imeanza kufanya maboresho ya kanuni na mwongozo wa biashara ya kaboni za mwaka 2022 ili ziwatambue na kuwanufaisha wakulima na wafugaji nchini.

Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Khamis Hamza Khamis, alibainisha hatua hiyo bungeni jana alipojibu maswali ya Mbunge wa Viti Maalum, Jacqueline Msongozi.

Alisema kanuni hizo zinalenga kuhakikisha jamii na wadau mbalimbali wanaohusika na biashara hiyo ikiwa pamoja na serikali kunufaika kikamilifu kutokana na faida zake.

Khamis alieleza kuwa katika mwaka wa fedha 2023/24, serikali imetenga fedha kwa ajili ya kutoa elimu ya mazingira kwa umma ikiwamo biashara ya kaboni.

Alisema ni matumaini ya serikali kwamba, kupitia jitihada hizo, wananchi watapata uelewa na kunufaika na biashara hiyo wakiwamo wakulima na wafugaji.

Naibu Waziri huyo pia alifafanua kuwa biashara ya kaboni ni moja ya mbinu za kupunguza uzalishaji wa gesijoto (mitigation) ambayo iliridhiwa katika itifaki ya Kyoto ikizitaka nchi wanachama kupunguza uzalishaji wa gesijoto iliyorundikana angani.

Pia alisema biashara hiyo iko katika masoko ya aina mbili ambayo ni soko la hiari/huria (voluntary carbon market) na Soko la Umoja wa Mataifa (official carbon market).

Pamoja na mwongozo huo, alisema tayari Ofisi ya Makamu wa Rais imetoa elimu kwa makundi mbalimbali ikiwamo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, wizara zote za kisekta na taasisi zake, wakuu wa wilaya wote, wakuu wa mikoa na makatibu tawala wa mkoa na kwa wadau mbalimbali.

Juni 19 mwaka huu, ofisi hiyo ilitoa semina kwa wahariri wa vyombo vya habari iliyolenga kujenga uelewa kuhusu kanuni na mwongozo wa biashara ya kaboni.

# China kuongeza nguvu utekelezaji miradi ya maji

**Na Joseph Mwendapole**

BALOZI wa China nchini, Chen Mingjian, ameahidi kuendelea kishirikiana na serikali kuboresha huduma za majisafi na usafi wa mazingira.

Alitoa ahadi hiyo juzi baada ya kutembelea na kukagua mtambo wa kuzalisha maji wa Wami ulioko Chalinze mkoani Pwani, unaosimamiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA).

Alisema anafurahi kuona kazi kubwa iliyofanyika kuongeza uzalishaji wa maji kutoka katika mtambo huo wa maji ambao ulijengwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na China.

Alisema Serikali ya China iko tayari kuendelea kushirikiana na Serikali ya Tanzania kuboresha miundombinu katika mtambo wa Wami ili utoe huduma bora zaidi kwa wananchi.

"Tunaipongeza DAWASA kwa hatua ilizozichukua za kutunza na kuboresha miundombinu pamoja na kufanya upanuzi wa mtambo. Hizi ni jitihada kubwa za kupongezwa, kwa kuwa zinalenga kutoa huduma kwa wananchi wengi," alisema Balozi Chen.

Akitoa maelezo kwa Balozi kuhusu chanzo hicho cha maji, Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Kiula Kingu. alisema ziara ya Balozi wa China imelenga kufuatilia maendeleo ya mtambo huo ulizinduliwa rasmi mwaka 2001.

Alisema nia ya ziara hiyo fupi ilikuwa ni kutembelea mifumo iliyojengwa miaka mingi iliyopita na baadaye kujadili maeneo muhimu ya ushirikiano kwa lengo la kukuza uhusiano baina ya mataifa haya mawili rafiki.

Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Exim India imefanya maboresho ya upanuzi wa uzalishaji wa mtambo wa maji Wami kutoka kuzalisha lita milioni 7.2 mpaka lita milioni 21 kwa sasa na kutoa huduma kwa wananchi 197,000 na vijiji 47.

Alisema mpaka sasa utekelezaji wa mradi wa Chalinze awamu ya tatu umefikia asilimia 95 na kazi iliyobaki ni kuweka mifumo ya TEHAMA ili kusimamia miundombinu ya mradi huo ambao unatoa huduma katika mikoa ya Pwani na maeneo ya mikoa ya Morogoro na Tanga.

"Mifumo hii ya TEHAMA itaiwezesha DAWASA kufuatilia mwenendo wa ujazaji maji katika matangi na usambazaji maji na lengo la maboresho haya ni kuhakikisha tunakuza upatikanaji wa maji katika maeneo ya mijini na vijijini yanayohudumiwa na mradi huu kwa asilimia 95 mijini na 85 vijijini," aliongeza.

Mwajuma Saidi, mkazi wa Msata, aliishukuru serikali kupitia DAWASA kwa kuwatua ndoo kichwani wakazi wote wa eneo lao.

"Kero ya maji ilikuwa kubwa hapa, tulikuwa tunafuata maji bondeni yenye chumvi ambayo hayakuwa salama kiafya, kwa sasa tunashukuru shida imeisha," alisema .

Mradi wa maji Chalinze awamu ya tatu umetekelezwa na DAWASA kwa lengo la kutoa huduma kwa wananchi 274,603 wa miji ya Chalinze, Morogoro, Pwani, Ngerengere na baadhi ya vijiji vya Wilaya ya Handeni mkoani Tanga.

# Mwenge wa Uhuru kukagua miradi ya bilioni 47/- Arusha

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, amesema katika mkoa huo Mwenge wa Uhuru utakagua na kuweka mawe ya msingi miradi 62 yenye thamani ya Sh. bilioni 47.29.

Mongella alisema hayo jana katika viwanja vya Shule ya Sekondari Tingatinga iliyopo katika Wilaya ya Longido, wakati akipokea Mwenge wa Uhuru kutoka kwa MKuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu.

"Katika Mkoa wa Arusha Mwenge wa Uhuru utakimbizwa kilomita 1168.47 utakagua miradi 62 yenye thamani ya Sh. bilioni 47.29," alisema.

Kwa mujibu wa Mongella Sh. bilioni 31,18 zilizotekeleza miradi hiyo zimetoka serikali kuu, Sh.bilioni 1.65 zimetoka halmashauri, Sh. bilioni 3,29 zimetoka kwa wahisani na Sh. biilioni 11.15 zimetoka kwa wananchi.

Aidha, Mongella alisema katika miradi hiyo 16 itawekewa mawe ya msingi yenye thamani ya Sh. bilioni 26.94 miradi 14 yenye thamani ya Sh. bilioni 11.20 itazinduliwa, miradi nane yenye thamani ya Sh. milioni 694.99 itafunguliwa na miradi 24 yenye thamani ya Sh. bilioni 8.45 itatembelewa na kukaguliwa.

Mongella alisema ajenda kuu ambazo zimezingatiwa katika Mkoa wa Arusha, ni pamoja na ulinzi wa mazingira, udhibiti wa maambukizi Virusi Vya Ukimwi (VVU), kupambana na rushwa pamoja na kupiga vita dhidi ya dawa za kulevya.

Mkimbiza Mwenge wa Uhuru Kitaifa, Abdalla Shaibu Kaim, alitoa rai kwa wakuu wa wilaya zote za Mkoa wa Arusha, kuhakikisha taarifa za miradi yote, inayotembelewa zinakuwa kwenye maeneo ya miradi.

# Maofisa kazi wanaotumia majina ya viongozi waonywa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SERIKALI imewanyooshea kidole maofisa kazi wafawidhi wanaotumia vibaya majina ya viongozi wa kiserikali, kutoa lugha za vitisho kwa baadhi ya waajiri ili kushawishi kupewa rushwa, wakati wakifanya ukaguzi sehemu za kazi.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako, amesema tangu ateuliwe kuiongoza wizara hiyo, amekuwa akipokea malalamiko ya baadhi yao kutuhumiwa kutumia vibaya majina ya Waziri mwenye dhamana pamoja na Kamishana wa Kazi, jambo ambalo linaitia doa mamlaka ya uteuzi.

Prof. Ndalichako, alikuwa akizungumza jana jijini Arusha, wakati akifungua mafunzo ya siku tano kwa maofisa hao, ambayo yamefadhiliwa na Shirika la Kazi Duniani (ILO).

"Mnapotumia majina ya wateule wa Rais mnashusha hata heshima ya Rais aliyetuteua, sasa nimeona leo niwaambie kuanzia sasa nikipata mtu ameenda mahali anatumia jina langu au Kamishana wa Kazi, nitaamrisha akamatwe mara moja na ashughulikiwe kwa mujibu wa sheria. Nawaomba achani tabia hiyo, kwa sababu mtapata taabu," alihadharisha.

Aidha, aliwasihi kubadilika na kutumia lugha za staha wanapotekeleza majukumu ya kazi zao wanapofanya ukaguzi kwa waajiri, huku akiwataka kuacha kubagua kufanya ukaguzi kwa waajiri wenye uwezo na kuwaacha wasio na uwezo, kwa kuwa kufanya hivyo hakutoi haki sawa kwa wafanyakazi na wanatengeneza mazingira ya rushwa.

"Sisi ni watumishi wa umma, hatuitwi mabwana wakubwa kazi yetu kutumikia wananchi na waajiri ili wahakikishe wanazingatia sheria za kazi kwa maslahi mapana ya wafanyakazi na siyo vinginevyo, kafanyeni ukaguzi kikamilifu na hapa kuna masuala mengi ya usimamizi wa kazi kama vile kuangalia utekelezaji wa kima cha chini cha mshahara kilichotolewa na serikali Januari Mosi mwaka huu, changamoto za mikataba wapo wanaofanya kazi bila mikataba ya kueleweka, mambo yapo mengi ya kusimamia.

"Tujitahidi kuipenda kazi yetu na kufanya kwa ushirikiano na vyombo vyote vya serikali vya masuala ya kazi, tukitanguliza weledi na uadilifu ambao ndio msingi wa kuepuka rushwa na kujenga mazingira ya rushwa kwa kuanzishwa majadiliano pale mnapogundua dosari kwa waajiri hasa wale wenye fedha acheni hiki kitu kinatushushia heshima wote," alisema.

Pia, alisema baadhi yao wanafanya ukaguzi hewa ambazo hawatoi taarifa sehemu yoyote, badala yake wanaanzisha majadiliano ili kujenga mazingira ya rushwa, ambayo haijawahi kujaa popote na shida haziishi sababu fedha ikipatikana na matumizi yanaongezeka.

Kadhalika, alionya baadhi yao kuvuka mipaka ya kazi kwa kwenda kufanya ukaguzi eneo ambalo siyo lake, kutolea mfano kwa baadhi yao kutoka Kinondoni kwenda Temeke au Ilala kufanya ukaguzi, kitu ambacho hakileti taswira nzuri ya kazi, isipokuwa wanavutwa na waajiri wenye fedha.

Awali, Mratibu wa Masuala ya Ukimwi na Usalama Sehemu za Kazi wa Shirika la ILO, Getruda Sima, alisema: "Mafunzo haya yanawawezesha namna bora ya kutumia mikataba ya kimataifa, pamoja na mkataba wa kufanya ukaguzi sehemu za kazi, kwa kuzingatia usimamizi wa haki sawa kwa waathirika wa UKIMWI i mahali pa kazi."



Mkuu wa Wilaya ya Mbulu mkoani Manyara, Kheri James, akizungumza na viongozi na wakazi wa Kata ya Haydom juzi, kuhusu ushirikishwaji wa kuchangia maendeleo na kusoma taarifa ya mapato na matumizi. **PICHA: GIFT THADEY**

# China yakabidhi EAC magari ya mil. 956/-

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

CHINA imetoa msaada wa magari manane aina ya pick up, kwa ajili ya kusaidia uendeshaji wa shughuli za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC), yenye thamani Dola za Marekani 400,000 (Sh. milioni 956).


Balozi wa China nchini Tanzania, Chen Mingjian, akizungumza jana jijini Arusha na menejimenti ya EAC, wakati wa hafla ya makabidhiano ya magari hayo, alisema msaada huo umetolewa baada ya kukwama kufanyika hivyo mwaka 2021, kutokana na janga la UVIKO-19 kuitikisa China.

"Mbali na kukabidhi magari haya, tumekuja pia na wataalamu wa kutoa mafunzo ya matumizi ya magari haya, kwa madereva na mafundi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ili yatakapoharibika wafahamu jinsi ya kutengeneza," alieleza.

Aidha, alisema China imekuwa ikishirikiana na nchi za EAC, katika masuala mbalimbali ikiwamo ujenzi wa miundombinu mbali mbali, sanjari na kusaidia kukuza demokrasia, uwajibikaji na utawala bora. "Tumekuwa tunasaidia katika nyanja mbalimbali kwa lengo la kukuza amani, demokrasia utawala bora na uwajibikaji, ili kusaidia wanachama wa EAC kupata huduma bora," alisema.

Naye Mwakilishi wa Katibu Mkuu EAC, Mkurugenzi wa Sekta ya Uzalishaji EAC, Irene Isaka, alisema Jumuiya ya Afrika Mashariki, imekuwa ikishirikiana na China katika masuala mbalimbali ya kijamii katika kukuza mtangamano.

Alisema: "Leo tumeletewa magari nane na tuna mabasi matatu yenye uwezo tofauti ambapo moja lenye uwezo wa kubeba watu 26 na hayo mawili watu 36 halafu pia wametuletea pick up, hivi vyombo vya usafiri ni muhimu sana kwa nchi za EAC kama mnavyofahamu sasa tuna nchi wanachama saba na kuna kazi mbalimbali katika jumuiya, hivyo msishangae kuona mabasi haya nchi mbalimbali."





# Waliovamia hifadhi wamegewa eneo la makazi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANANCHI wa vijiji sita wilayani Shinyanga ambao wamevamia Hifadhi ya Msitu wa Nindo uliopo wilayani humo, wamemegewa eneo la makazi ndani ya hifadhi hiyo lenye ukubwa wa hekta 3,726 ili kupisha maeneo mengine ambayo yataendelea kuwa sehemu ya hifadhi.

Hifadhi hiyo ya Msitu wa Nindo ilitambuliwa kisheria na kutangazwa na Gazeti la Serikali Namba 10 mwaka 1958, likiwa na ukubwa wa hekta 27,446, lakini baada ya wananchi kuvamia na kuishi eneo la hifadhi limesalia hekta 10,969.

Mhifadhi Mkuu Daraja wa Pili kutoka Wakala wa Huduma ya Misitu Tanzania (TFS) Kanda ya Magharibi, Lucas Nyambala, alibainisha hayo juzi kwenye kikao cha kujadili utekelezaji wa maamuzi ya mawaziri nane wa kisekta juu ya utatuzi wa mgogoro wa hifadhi hiyo.

Alisema katika utatuzi wa mgogoro huo serikali kupitia mawaziri hao iliamua kumega eneo ndani ya hifadhi hiyo ya Msitu Nindo lenye ukubwa wa hekta 3,726 kwa ajili ya makazi na hekta 7,243 zibaki kusimamiwa na Mamlaka ya Misitu Tanzania (TFS) kwa ajili ya uhifadhi.

"Vijiji sita ambavyo vimevamia eneo la Hifadhi ya Msitu wa Nindo ni Ng'homango, Mwabundala, Lyamidati, Kadoto, Mwajiji na Buzinza, ambako wananchi wanapaswa kuachia maeneo haya ya uhifadhi na kwenda kuishi katika eneo ambalo wamemegewa na serikali ndani ya hifadhi hiyo," alisema Nyambala.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, alimpongeza Rais Samia kwa kutenga eneo ndani ya hifadhi hiyo ya Msitu wa Nindo kwa ajili ya makazi ya wananchi, huku akiwasihi wananchi ambao wanapaswa kupisha maeneo mengine ya hifadhi waridhie kuondoka na kuishi eneo ambalo limetengwa kwa ajili yao.

Wajumbe wa kikao hicho wakitoa maoni yao kwenye majadiliano hayo walisema kabla ya wananchi kuanza kuhamishwa wapewe elimu kwanza juu ya kupisha eneo ambalo limesalia kwa ajili ya uhifadhi na baada ya kupisha maeneo hayo yawekewe alama za mipaka ili kusijitokea uvamizi tena.



Ofisa Elimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema, Amani Tangalo (katikati), akikata utepe kuzindua choo cha matundu 12 kilichojengwa na mgodi wa uchimbaji madini wa Sotta Mining Corporation Ltd (SMCL), katika Shule ya Sekondari Busisi, wakati wa uzinduzi na makabidhiano ya vyoo hivyo, wilayani humo, mkoani Mwanza jana. Kushoto ni Diwani wa kata ya Busisi, Dickson Samuel na Mkurugenzi na Meneja Mkuu wa mgodi huo, Damien Valente. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# DC afichua mbinu mpya utoroshaji dhahabu

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKUU wa Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, Mboni Mhita amefichua mbinu mpya inayotumiwa na baadhi ya wafanyabiashara kutorosha dhahabu kuwa ni pamoja na kutoa taarifa ambazo siyo sahihi katika ofisi za madini hali inayosababisha upotevu wa mapato serikalini.

Mhita aliyabainisha hayo juzi wakati wa ziara yake ya kushtukiza katika Soko Kuu la Dhahabu Kahama na Mwime yaliyopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama na kusema kuwa hatavumilia kuona vitendo hivyo vikiendelea wilayani humo.

Alisema baadhi ya wafanyabiashara wamekuwa siyo waadilifu na wanashirikiana na wachimbaji wadogo kuibia serikali mapato yatokanayo na madini wanatoa taarifa ambazo siyo sahihi za viwango vya madini walivyonavyo katika ofisi za madini zilizopo sokoni na wanapokaguliwa wanakutwa na madini mengi jambo ambalo ni kinyume cha sheria.

"Katika ofisi za madini mnasajili kuwa na gramu 200 za madini huku mfukoni mnakuwa na kilo moja ya dhahabu, huu ni wizi na hatutauvumilia na atakayebainika tutamchukulia hatua za kisheria," alisema Mhita.

Aidha alisema ili kuondoa wizi huo kunatakiwa kujengwa kwa ukuta wa kutenganisha soko la madini na ofisi za umma zilizopo kwani eneo hilo kuna ofisi za umma nyingi na kumwagiza Mkurugenzi wa Manispaa ya Kahama, Anderson Msumba kwa kushirikiana na ofisi ya madini kujengwa ukuta huo.

Pia aliwataka viongozi wa wachimbaji wadogo na wasimamizi wa masoko ya dhahabu kuhakikisha wanasimamia na kudhibiti utoroshaji wa madini katika maeneo yao na kutoa taarifa kwa baadhi yao watakaobainisha kushiriki na kuisababishia serikali kukosa mapato ili wachukue hatua za kisheria ikiwemo kufutia leseni zao.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Clemensi Mkusa alisema ofisi yake itajenga uzio huo wa kutenganisha soko hilo na ofisi mbalimbali za umma zilizopo katika eneo hilo kuwa na geti moja na watakaokuwa wanaingia sokoni na kutoka watakuwa wanafanyiwa ukaguzi wa mara kwa mara.

Alisema wanatarajia kujenga soko jipya la madini Kahama ambalo litakuwa la ghorofa nne ambalo litawaweka wanunuzi wadogo na wakubwa sehemu moja na mianya hiyo ya utoroshaji itakuwa imedhibitiwa.

Alisema kwa sasa wako katika hatua za mwisho za kupitisha mchoro wa jengo hilo.

Ofisa Madini mkazi wa Mkoa wa Kimadini Kahama Mhandisi Jeremiah Hango alisema, hivi karibuni waliwakata wafanyabiashara wanne wa madini na kuwafungia ofisi zao kwa kutoa taarifa zisizo sahihi za viwango vya madini, kabla ya kuingia sokoni na mali zao wamezikabidhi Benki Kuu ya Tanzania na kesi zao zinaendelea mahakamani.

Katibu wa Soko la Madini Mwime, Nila Francis alisema, utoroshaji huo unaanzia kwa wachimbaji wadogo kabla ya kufika sokoni, wanafika na viwango vidogo vya madini sokoni kwa lengo la kutaka kujua bei huku kiwango kikubwa kikiwa mifukoni.

Hivyo aliiomba serikali kutoa elimu ya viwango vya bei ili kuondoa tatizo hilo.

# Jaji Mkuu: Misaada dhidi ya Mahakama inaongeza ufanisi

**Halima Ikunji,** TABORA

JAJI Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahimu Hamisi Juma ambaye pia ni Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Mahakama amesema anatambua misaada inayotolewa na wadau wa Mahakama Kuu kupitia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Tabora kwamba imekua ikisaidia kuongeza ufanisi katika utendaji kazi hususani katika mfumo wa TEHAMA.

Alitoa kauli hiyo juzi wakati wa utoaji wa vifaa vya TEHAMA uliokabidhiwa na Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Balozi Dkt.Batrida Buriani katika Mahakama Kuu Kanda ya Tabora vyenye thamani ya zaidi ya Sh.milioni saba na kusema kuwa jitihada hizo zitaisaidia Mahakama kuongeza ufanisi katika utoaji haki.

Prof. Ibrahimu alisema kuwa wadau ni watu muhimu katika maswala ya maboresho ya Mahakama na vifaa hivyo vimeweza kusaidia wananchi kupata huduma kwa haraka kupitia mfumo wa TEHAMA.

"Tume haiwezi kusimama peke yake bila masikio na macho ya wajumbe wa kamati za maadili za mkoa na wilaya kwa kushirikiana katika kuboresha Mahakama zetu. Hivyo mapendekezo ya Tume ya Utumishi ni kuhakikisha utendaji kazi unaendana na maadili ya kazi husika,"alisema.

Naye Jaji Kiongozi na Kamishna wa Tume ya Utumishi wa Mahakama, Mustapher Siyani alisema ushiriki kwa viongozi wa serikali katika ujenzi wa imani ya mwananchi kwa Mahakama ni muhimu ili kuisaidia mhimiri huo kutekeleza shughuli zake.

ama

ALHAMISI JUNI 8, 2023

AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**Watoto wanaotamani udaktari wapelekwa kuzuru Muhimbili**



Ukurasa 13

Dawa za kulevya zinavyobaki sumu ya afya jamii nchini, hadi duniani



Ukurasa 14

**SUA yabuni kifaa Smart TB, cha kumsaka mgonjwa asiyepo kliniki**

UTEKELEZAJI MBIU YA RAIS SAMIA...

# Wizara ya Afya harakati zimepamba teknolojia kukusanya mazao damu

- Njia mpya ya kuwezesha ziada ya benki
- Kila hospitali rufani kuwa na kituo chake

**Na Yasmine Protace**

INAFAHAMIKA, damu ni muhimu kwa binadamu na inapaswa kuwamo mwilini ikiwa safi na salama. Hiyo ndiyo sababu katika hospitali kubwa ni kanuni sasa kuwa na benki ya damu na kitaifa kuna vituo maalum vya benki ya damu, kwa ngazi tofauti hata kufikia kwenye kanda.

Kwa mujibu wa Mpango wa Taifa wa Damu Salama, kunakusanywa damu kutoka kwa wachangiaji wa hiari ikifanyika kwa njia kuu mbili; uchangiaji wa damu nzima, pia kuchangia mazao mahsusi ya damu (apheresis donation).

Katika eneo hilo la pili, mchangiaji anatoa damu kwa sehemu maalum kama vile katika tafsiri ya kitaalamu; chembe sahani (platelets), sehemu ya majimaji ya damu (plasma) au seli nyekundu (red blood cells).

Ni eneo ambalo tangu aingie madarakani, imo katika vipengele vya maendeleo ya afya, ambavyo Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, analisisitizia ikiendana na programu mpya ya Utalii Tiba na usalama wa mama na mtoto.

Ni hali inayoendana na maboresho ya mihimili ya matibabu, hasa katika hospitali kubwa, ikiwamo Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, Dar es Salaam na Hospitali ya Benjamin Mkapa, jijini Dodoma.

Sasa, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, anasifu ni mafanikio yanayoendana na sera za Rais





Washiriki katika tukuop la kuchanngia akiba katika Benki ya Damu. **PICHA: MTANDAO**

Dk. Samia anapochukua jukumu kwajibikia eneo la damu safi na salama, kununua na kusambaza mifuko ya kukusanya damu bure kitaifa kila nchini.

Kwa mujibu wa Ummy, ni hali inayohakikisha kukosekana upungufu wa mifuko ya kukusanya damu katika vituo vyote kwa wakati wote.

Mara zote, utengenezaji damu salama katika hospitali zote za rufani na mikoa, inatajwa kusaidia ipatikane kwa wingi na katika hali salama, kuhusu kada ya waathirika kama wajawazito na watoto.

**MENEJA DAMU**

Katika kutekeleza maelelekezo hayo ya Rais Dk. Samia, Kaimu Meneja Mpango wa Mpango wa Taifa wa Damu Salama Dk. Abdul Juma Bhombo, anasema sasa hospitali za rufani za kanda na mikoa zitaanza kuzalisha mazao ya damu, kuimarisha upatikanaji wa huduma ya damu safi na salama nchini.

Ni tamko lake katika uzinduzi wa kampeni mojawapo ya kuhamasisha na kuchangia damu safi na salama hivi karibuni, akifafanua kuwa katika kuitikia wito wa mwelekeo wa rais, Wizara ya Afya kupitia Mpango wa Taifa wa Damu Salama, ambayo imeanza utekelezaji wa kuongeza wigo wa kutengeneza mazao damu kwa kuhusisha hospitali za rufani mikoa na kanda.

Anasema, awali kazi hiyo ilifanyika katika vituo vya Damu Salama-Kanda. Hadi sasa, hospitali zilizokwishajengewa uwezo wa kutengeneza mazao ya damu zinatajwa ni za mikoa ya Geita, Simiyu, Iringa na Arusha-Mount Meru.

Pia, Dk. Juma anataja katika orodha hiyo, vituo vikubwa vya afya kitaifa, zimo hospitali za Benjamin Mkapa, pia zingine za Dar es Salaam; Mloganzila, Taasisi ya Mifupa-MOI, CCBRT na Hospitali ya Taifa Muhimbili, kukifanyikia uzalishaji wa moja kwa moja wakati mtu anapochangia damu, kulingana na mahitaji ya kituo.

Aidha, meneja huyo anasema Mpango wa Taifa wa Damu Salama, umeanzisha uchangiaji damu kwa njia ya 'Apheresis' ambayo mtu anatoa aina fulani ya mazao ya damu yanayohitajika.

Dk. Juma anaeleza:"Hii ni teknolojia mpya na itawezesha upatikanaji wa mazao ya damu yenye viwango na ubora na yataongeza ufanisi wa matibabu kwa wagonjwa wanaoongezewa damu hasa wagonjwa wa saratani.

"Mafanikio haya yanatokana na uwezeshaji wa Serikali ya Awamu ya Sita hasa katika ununuzi wa kununua mashine za

**INAENDELEA UK.14**

AFYA

# Watoto wanaotamani udaktari wapelekwa kuzuru Muhimbili, wakihamasika maradufu

• Wenye fani wawaanikia njia za kupita kuyaona mafanikio



Mkuu wa Ukunga na Afya ya Uzazi, katika Hospitali ya Taifa Muhimbli, Priscilah Kinyamagoha (kushoto) akizungumza na wanafunzi ziarani hospitalini hapo, siku chache zilizopita kushuhudia kinachofanyika hapo, ikiwa ni sehemu ya hamasa yao, wakipelekwa na Shirikisho la Vikundi vya Ujasiriamali Tanzania (SHIVUTA). **PICHA: HALFANI CHUSI**

**Na Halfani Chusi**

'MTOTO unavyomlea, ndivyo anavyokua,' ni usemi mkongwe ambao umetumiwa kwa mafanikio na Shirikisho la Vikundi vya Ujasiriamari Tanzania (SHIVUTA), jijini Dar es Salaam, kupitia mradi wake 'binti kinara kuwawezesha wanafunzi.'

Msingi wake ni mradi mahususi wa kuwawezesha watoto wanaotoka katika mazingira magumu kwenye maeneo tofauti nchini, kwa kuwafadhili kimasomo na kuwapa usimamizi wa kile wakipendacho hadi kuyafikia malengo yao.

Katika kutimiza azma hiyo, wanafunzi waliofadhiliwa na mradi huo, hasa wanaopenda fani ya udaktari, waliwapeleka katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Dar es Salaam, lengo ni kuwakutanisha na madaktari bingwa wajifunze na kuhoji siri ya mafanikio yao.

Ni aina ya kujifunza kama iliyotumiwa na mwanazuoni, Jerome Bruner, kwamba kuna njia ya kujifunza kwa vitendo na ndio ilitumiwa na wanafunzi, kuwandaa katika njia ya vitendo kuelewa safari yao.

Baada ya kuwasili hospitalini hapo, geni wa wanafunzi hao wakiwa na jopo linaloongozwa na Mkurugenzi wa Shivuta, Andrew Koti, hapo wakapokewa kwa bashasha na vigelegele kutoka kwa madaktari bingwa hospitalini hapo, huku vichwani mwao wakifahamu ndio warithi wa baadaye, wakionyesha kuwapenda na kuwapa ushirikiano.

> **Tumewaleta hapa hospitalini kwa sababu kuna ,madaktari bingwa wengi na wataalamu kwa hiyo tunaamini ziara hii itawafanya watoto wasome kwa bidii na kutimiza malengo.**

Hapo wakapewa chumba maalumu na punde kidogo akaletwa daktari bingwa wa masuala ya uzazi na mara moja, wanafunzi waliokuwa na bashasha ya kuuliza maswali ya wanachokitamani kuhusu masuala ya afya ya uzazi na uuguzi, wakaanza kuhoji maswali.

Ni mjadala wa majibu na maswali, uliochukua zaidi ya saa nne, wakipewa majibu ya papo kwa hapo na daktari mhusika, ikiwa ni pamoja na kupata simulizi ya maisha aliyopitia daktari huyo mpaka akafanikiwa.

Kimsingi, ni hadhira iliyowavutia wanafunzi hao na hata wakatamani moja kwa moja kusoma kwa bidii, ili kufikia malengo ya kuwa madaktari bingwa, kama ilivyokuwa kwa daktari huyo.

Nipashe iliyokuwa bega kwa bega kwenye tukio hilo, ikashuhudia wanafunzi hao wakifundwa kusoma kwa bidii na kuepuka vishawishi, ikiwamo mimba za utotoni na kuolewa wakiwa na umri mdogo na kwamba wanapaswa kutambua, dunia ya sasa inataka mtoto asome kwa nadharia na vitendo kwa kile anachokipenda.

Mwanafunzi wa Darasa la Sita, ambaye ni miongoni mwa waliohudhuria ziara hiyo mwenye ndoto ya kuwa Daktari Bingwa wa Uzazi, Sonia Chilani, anasema jambo hilo limewatoa tongotongo na kwamba sasa wanapaswa kusoma kwa bidiii ili kufikia hatua hiyo.

Anashauri serikali kuweka mkakati wa kuwapeleka wanafunzi hata walioko ngazi za chini kwenye taasisi ambazo wanatamani kusomea.

"Nimewaona madaktari wa kike zamani nilikuwa ninajua madaktari ni wa kiume tu, hili ziara imeniongezea hali ya kujituma na nitapambana na nitasoma kwa bidii mpaka nije kuwa daktari bingwa" anasema mwanafunzi huyo, kutoka Shule ya Msingi Serengeti ya Dar es Salaam.

**MALEZI WAO**

Mlezi wa watoto hao kundi la Binti Kinara, ambaye pia ni Mshindi wa Miss Tanzania, Juliana Lugumisa, anasema limekuwa jambo kubwa kwao, kwa kuwa watoto hao wamepokewa vizuri na wamezungushwa maeneo tofauti katika hosipitali hiyo, ili kuyaona yote.

Anaeleza imani yake kwamba, jambo hilo litakuwa chachu kwao kujituma kufanya kazi kwa bidii, ili waweze kufikia malengo ya kuwa madaktari bingwa nchini.

"Wenzetu wazungu wana utamaduni wa kumpeleka mtoto kwenye shule ambayo kuna fani anayotaka kusomea na sisi tumeona tuige mfano huo tumewaleta hapa (MNH) Upanga, wamekutana na madaktari bingwa wameuliza maswali mengi na wamehamasika.

"Tuna imani watasoma kwa bidii, ili wafikie ndoto hiyo, tumetembelea majengo ya dharura, moyo, afya ya uzazi, hii itasaidia mtoto kupata morali ya kusoma kwa bidii," anasema Juliana

Anaendelea kubainisha watoto hao walichokiokota akitamka: "Sio kila mwanamke ni nesi, wengine ni madaktari. Kwa hiyo, wamefuta ile dhana kuwa mwanamume ni daktati na mwanamke nesi, kwa sasa wanaelewa kuwa hata mwanamke anaweza kuwa daktari"

Mratibu wa Shivuta, Paulo Chegere anasema mbali na kufadhili wanafunzi wanatoka kwenye maisha magumu pia wanasimamia na kuhamasisha vikundi vya kuweka fedha na kukopa, kutoa elimu ya fikra chanya kitaalamu, hapo anafafanua kuwa walichโlengea ni kuwapa watu uwezo wa kujitegemea na kuitumia akili vizuri kutatua changamoto zinazo wakabili.

Anaendela kuwa, jambo jingine wanalolifanya ni kusaidia watu wenye uhitaji maalumu na kuwapa nafasi ya kufikia malengo yao licha ya ulemavu walionao.

"Kazi ya mradi wa binti kinara ni kumuibua mtoto wa kike anayefanya vizuri kwenye masomo, ili aje kutimiza ndoto zake na kuwasaidia wengine.

"Tumewaleta hapa hospitalini kwa sababu kuna ,madaktari bingwa wengi na wataalamu kwa hiyo tunaamini ziara hii itawafanya watoto wasome kwa bidii na kutimiza malengo,"anasema Chegere

**MKUU WA UKUNGA**

Mkuu wa Idara ya Ukunga na Afya ya Uzazi Hospitali ya Muhimbli, Priscilah Kinyamagoha, anayeonyesha kufurahishwa na ujio wageni hao ofisini kwake, anasifu jambo hilo kwao imekuwa fursa na furaha kubwa na kwamba, ni hali itakayowajenga na kuwapa morali wanafunzi, wasome kwa bidii zaidi.

Anasema ni jambo linalopaswa kuigwa na shule nyingine, ili watoto wanaotamani kuwa madaktari waweze kufanya maamuzi sahihi wangali wadogo.

"Hii ni chachu kwa wanafunzi wengine na serikali kwa ujumla, waweze kuwapeleka wanafunzi kwenye maeneo ambayo watoto wanatamani kuwa.

"Kujionea kama ni jeshini, wapelekwe kwenye kambi za jeshi, kama ni urubani wapelekwe kwenye viwanja vya ndege, kama ni hospitali waletwe ili wajifunze na waone namna kazi wanayotamani kuwa inavyofanyika," anashauri mtaalamu huyo

AFYA

HEROINI NA BANGI ZIKITIKISA...

# Dawa za kulevya zinavyobaki sumu ya afya jamii nchini, hadi duniani

• Pata alichoanika waziri, wadau wa UN

**Na Zanura Mollel**

DAWA za kulevya aina ya heroine zinatajwa kutengenezwa na kemikali ya 'morphine' inayopatikana kwenye utomvu wa tunda la mmea unaolimwa zaidi nchi za Afghanstan, Myanmar na Laos.

Vilevile inatajwa kuenea katika mapori ya nchi za Burma, Los Vietnam, Uthai, Afghanistan, Pakistani na Uajemi.

Huwa inatumika sana duniani, ikilimwa kwa wingi kwenye nchi hizo, kutokana na udhibibiti duni wa kiserikali.

**NCHINI TANZANIA**

Tanzania nako kuna shida ya dawa za kulevya, hata kutoa mzigo kwa nchi kutenga bajeti ya kuwatibu waraibu wake, kuwaelimisha, pia kuendesha operesheni za kudhibiti usambazaji na usafirishaji haramu.

Kwenye nchi zilizoendelea, kuna matukio ya kihalifu yanayovuka mpaka, ikiwamo usafirishaji dawa hizo, ilhali nchini zinaingizwa dawa za kulevya kupitia mipaka isiyokuwa rasmi, wavushaji wakitumia pikipiki, baiskeli, mnyama punda,wanawake na watoto.

"Wakati mwingine Tanzania ni 'destination point' (ukingo wa kuvuka) wahalifu wa matukio mbalimbali, ikiwamo usafirishaji haramu wa dawa za kulevya kuelekea Afrika Kusini, pamoja na mataifa mengine," anatamka ofisa wa kiserikali, anayehusika na dawa za kulevya, hakupenda kutaja jina.

Nchini mwaka 2018, alikamatwa Mmarekani (jina tunalo) akiwa na kilo 2.188 za dawa za kulevya na akafikishwa kwenye Mahakama Kuu alikohukumiwa kifungo cha jela miaka 20, baada ya kutiwa hatiani kwa kosa hilo.

Kamishna wa Kinga na Tabia ,Mamlaka ya Kuzuia na Kudhibiti Madawa za Kulevya, Dk.Peter Mfisi anasema katika kukabili hayo, serikali imejenga vituo 15 nchini, ikitoa huduma kwa waraibu wa dawa ya kulevya.

Anataja sasa kuna waraibu 15,400 walioathiriwa na dawa za kulevya, ikiwamo heroine, wanaendelea kupatiwa matibabu.

**MTANDAO WA DCEA**

Kupitia tovuti inayoitwa DCEA, heroine inatajwa kushika nafasi ya pili kwa matumizi, baada ya bangi na inatumika kwa njia ya uvutaji, ikichanganywa na bangi kidogo, pia sigara inayonuswa au kujidunga.

Heroine ni kati ya dawa za kulevya zinazoongoza kudhuru kiafya na vifo vinavyotokana na kuzidisha matumizi yake, ikiwa juu kwa idadi ya watumiaji na vijana wengi wa nchini walioko ughaibuni, wako rehani au maarufu 'bondi' wakihatarisha maisha yao na taswira ya nchi kwa jumla.



Mtumiaji dawa za kulevya akijihudumia kwa sindano. **PICHA: MTANDAO**

Biashara ya dawa za kulevya, pia huambatana na uhalifu mkubwa wa kijamii kama ujangili, biashara ya binadamu na silaha, utakatishaji fedha, utekaji, ugaidi pia ngono.

**ILIVYO KIMATAIFA**

Ripoti ya Dawa Duniani, iliyotolewa na Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Madawa ya Kulevya na Uhalifu (UNODC) mwaka jana, inaeleza kuongezeka utengenezaji na soko kimataifa, ikiwamo nchini Afghanistan, ikuwajumuisha wanawake.

Ripoti inaeleza kuongezeka kilimo cha zao hilo nchini Afghanistan, ikikadiriwa wastani wa theluthi moja, bei nayo inapaa kwenye taifa hilo.

Abel Basutu, Ofisa Mwandamizi wa Mpango wa Dawa za Kulevya, pia katika Tume ya Umoja wa Afrika, anaelezea athari na rekodi mpya ya kuongezeka dawa aina cocaine inayotengezwa Afrika, sasa kukiwa kitovu cha kupitishwa dawa za kokeini.

Anashauri haja ya kupitishwa sera ya dawa za kulevya, inayosisitiza kudhibiti inavyosambazwa, pia matumizi yake, akitamka:"Kuimarisha haki ya makosa ya jinai na mifumo ya utekelezaji wa sheria, ili kuzuia uhalifu wa baharini na usafirishaji wa dawa za kulevya."

Daniel Brombacher, anayeongoza ubia wa sera ya kimataifa ya dawa za kulevya, katika Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Ujerumani (GIZ), anaeleza athari za dawa hizo kimazingira mitaani na kwa jamii, kwamba katika nchi zenye kilimo chake kikubwa, kuna athari zaidi, akitumia mfano wa kuhusishwa moja kwa moja na ukataji miti.

Pia, anataja madhara kwenye maji, udongo, na viumbe hai, Brombacher akielezea "asili ya 'kaboni' ya 'kokeini' ni mara nyingi zaidi ya ile ya miwa au hata ya maharagwe, hivyo maendeleo mbadala yana jukumu la kukabiliana na athari za hali ya hewa."

Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Madawa na Uhalifu (UNODC), inataja vifo vitokanavyo na kutumia dawa za kulevya, vimeongezeka katika muongo uliopita, Mkurugenzi Mtendaji wake, Ghada Waly, katika ripoti yake akifafanua mapya ya virusi vya Ukimwi.

Anataja watu wazima vifo vyao vimepungua karibuni duniani kote, lakini kwa watumiaji dawa za kulevya ni vingi, wanafikia asilimia 10 ya waathirika wapya katika miaka ya karibuni.

Anataja tofauti za kitaifa kwa kutumia mfano linganishi: "Wataalamu wa matibabu Afrika Magharibi na Kati katika mwaka 2019 walikuwa na wanatoa dozi nne za maumivu kila siku kwa wakazi milioni moja, wakati Amerika ya Kaskazini, idadi ya vipimo ilikuwa karibu 32,000".

> **Kiasi hicho ni mara tatu ya kiasi kilichokamatwa mwaka 2020. Aidha, katika kipindi hicho kiasi cha gramu 811.30 za cocain zilikamatwa.**

**TAARIFA ILIYOPO**

Mnamo Juni 10 mwaka jana, aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu George Simbachawene, akawasilisha bungeni Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya nchini, akitekeleza Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya.

Hapo Simbachawene akafafanua: "Kifungu hicho kinaweka masharti kwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, kuandaa na kuiwasilisha bungeni kila mwaka taarifa ya hali ya dawa za kulevya nchini."

Waziri anaitaja inawafahamisha wananchi hali ya dawa za kulevya kitaifa na kimataifa, jitihada za kiserikali, pia taasisi zake kukabiliana nayo, ushirikiano wa Tanzania na nchi zingine na changamoto zilizopo.

"Kwa upande wa dawa za kulevya zinazozalishwa viwandani mwaka 2021 jumla ya tani 1.13 za heroin zilikamatwa. Hiki ni kiasi kikubwa kuwahi kukamatwa kwa mwaka mmoja katika historia ya nchi yetu. "Kiasi hicho ni mara tatu ya kiasi kilichokamatwa mwaka 2020. Aidha, katika kipindi hicho kiasi cha gramu 811.30 za cocain zilikamatwa," anasema.

Anataja kuwa mara ya kwanza, mwaka 2022 katika historia ya mapambano dhidi ya dawa za kulevya, shehena kubwa kilo 430.77 dawa aina'methamphetamine' zilikamatwa ikihusisha wanaume tisa raia wa Iran.

Anafafanua, serikali imeendelea kupanua wigo wa matibabu kwa waraibu na hadi Desemba, mwaka 2021 huduma za tiba zilipatikana kwenye vituo 15 na jumla ya waraibu 11,650 walisajiliwa.

**MADHARA KIAFYA**

Inatajwa heroini inachangia kuongezeka magonjwa kama ya moyo, ngozi, figo, ini, mapafu, meno na kupoteza uwezo wa asili, pia ikiwa ni chanzo cha saratani mbalimbali mwilini, huku matumizi holela ya kujidunga) sindano, nayo inakaribisha maambukizi ya Ukimwi.

Mengine yanatajwa ni kukosa hamu ya kula, kudhoofu kiafya, upungufu wa maji mwilini kunakosababisha kukosa choo, mishipa ya damu kusinyaa au kupotea kutokana na udungaji sindano, mikasa ya vifo na umasikini.

AFYA

# SUA yabuni kifaa Smart TB cha kumsaka mgonjwa asiyepo kliniki

**Na Pendo Thomas,** MWANZA

CHUO Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA), cha Morogoro, kiko kwenye hatua za mwisho za ubunifu wa mfumo wa kifaa kiitwacho Smart TB, kinachosaidia kuvumbua na ufuatiliaji matibabu ya wagonjwa wa kifua kikuu nchini.

Hiyo ni mahsusi kwa wagonjwa ambao wamekuwa wakikatisha matibabu na kusababisha usugu wa dawa, hata wakawaambukiza wengine. Akieleza kuhusu mfumo huo unaolenga kusaidia wagonjwa na watoa huduma za afya, Mhadhiri wa SUA Dk. Joan Jonathan, anasema ni mfumo wenye uwezo wa kumtumia ujumbe mgonjwa kwenye simu yake ukimkumbusha kuhudhuria kliniki, siku moja kabla ya tarehe anayotakiwa kufanya hivyo.

Pia, ni mfumo utakaokuwa na uwezo wa kumtumia ujumbe kwenye simu mhudumu wa afya upande wa kifua kikuu, kufuatilia mahudhurio ya kliniki kwa wagonjwa siku moja baada ya tarehe anayotakiwa mgonjwa kufika hospitalini, ikitajwa ni hatua itakayosaidia kuwatambua wagonjwa wasiofika kwenye huduma na wakafuatiliwa.

"Mfumo huu unafanya kazi katika simu za aina zote na ujumbe utakuwa unasema 'ndugu fulani, unakumbushwa kuhudhuria kliniki fulani kupata matibabu' na kujua maendeleo ya afya yako" anasema Dk. Joan.



Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), Dk. Joan Jonathan, akitoa darasa la ubunifu wa kifaa kinachofanya ufuatiliaji wa nyendo za mgonjwa kliniki,mjini Mwanza. **PICHA: PENDO THOMAS**

Mtaalamu huyo anaeleza utasaidia kupunguza idadi ya wagonjwa wanaoshindwa kumaliza dawa za kifua kikuu, hivyo kupunguza vifo vitokanavyo na ugonjwa huo, vilevile ikidhibiti maambukizi mapya ya ugonjwa kifua kikuu, Tanzania.

Muda wa utafiti wa mfumo wa Smat TB, unafadhiliwa na SUA kwa kipindi tangu kuanzia Juni 2021, hadi Mei 2023 na baada ya kukamilika kwa taratibu zote, unaweza kuanza kusaidia sekta ya afya katika kuboresha utoaji huduma za matibabu upande wa kifua kikuu.

"Tunaomba Wizara ya Afya na wadau wengine wa masula ya afya, waupokee vyema mfumo huu, ili tupunguze idadi ya wagonjwa wanaositisha matibabu ya ugonjwa wa kifua kikuu,"anatamka Dk. Joan.

Ofisa Programu wa mfumo huo wa Smart TB kutoka SUA, Sharif Hamis, anasema katika mchakato wa ukamilishaji wake, wameujaribu mfumo katika maeneo mbalimbali, ikiwamo hospitali za Mazimbu na Hospitali ya Mkoa wa Morogoro, hata wakawakutanisha wataalamu wa sekta ya afya mkoani Mwanza kutoa maoni yao kuhusu uboreshaji wa baadhi ya vipengele katika mfumo huo.

Hamis anaeleza, kwa sasa mfumo huo uko kwenye hatua ambayo mtu wa kawaida hawezi kuufikia kwani una ulinzi ambao mtu asiye mhusika, hawezi kuingilia hata kufanya taarifa za mgonjwa na maendeleo yake yataendelea kuwa siri, baina yake na mtoa huduma za afya.

Pia, anaeleza kwamba ujumbe kwa mgonjwa utakaotolewa na mfumo hautakuwa wazi kutaja aina ya ugonjwa mtu anaoumwa, bali utaendelea kutunza faragha ya matibabu kwa muhusika, ukiwa na lengo la kutoa suluhisho la muda mrefu kuhusu ufuatiliaji.

**MWANZA WALIVYOUPOKEA**

Janeviv Patrick, Muuguzi katika Hospitali ya Mkoa wa Mwanza, Sekou Toure, anasema baadhi ya wagonjwa ni vigumu kuwafuatilia, hivyo kunachangia kusitishwa matibabu yao, hata wakazungumzia hatua ya mfumo mahsusi ufuatiliaji pande zote mbili, tabibu na mgonjwa, lengo ni kusaidia tija katika tiba.

Cosmas Dario, Mratibu wa Kifua Kikuu Wilaya ya Ilemela, anasema mfumo huo uliotambulishwa kwao, anaamini utawapa nafuu watoa huduma za afya katika kufuatilia maendeleo ya mgonjwa, akilinganisha tofauti yake na mifumo mingine mingi, wa sasa Smart TB umezingatia vipengele jumuishi kati ya wagonjwa na watoa huduma za afya, ambavyo mfumo wa.

"Huu mfumo naona umekuja kuboresha zaidi, unaweza ukawa msaada katika utoaji huduma na ufuatiliaji wa wagonjwa wa kifua kikuu," anatamka Dario.

Anaeleza uzoefu wake katika kitengo hicho, ni kwamba kuna wagonjwa wengi wanapotea kabla ya kumaliza matibabu na hata wanapofuatiliwa, hawapatikani, hivyo matumizi ya mfumo huo unaojumuisha watoa huduma,wagonjwa na watu wao wa karibu anaamini utasaidia kudhibiti.

## Wizara ya Afya harakati zimepamba teknolojia kukusanya mazao damu

**INATOKA UK.11**

kisasa za 'apheresis' na vifaa tiba vingine vya kutengenezea mazao ya damu."

Meneja huyo anasema, mahitaji ya sasa ya damu yanapatiwa majibu kiwango cha asilimia 76, ambayo Wizara ya Afya imeweka malengo kukusanya chupa 550,000 za damu ambazo ndio mahitaji kitaifa kila mwaka.

Anataja mkakati wa Mpango wa Damu Salama kuwa ni kufanyika uhamasishaji wa kuchangia damu salama katika sherehe za serikali kitaifa, hasa kwenye mikoa ya Dar es Salaam, Kigoma, Mbeya, Morogoro, Mwanza na Iringa.

**WAZIRI AFYA**

Waziri Ummy, katika kilele cha Siku ya Mchangia Damu Duniani tarehe 14 mwezi huu, iliyoendana na kuzindua jengo la Mpango wa Taifa wa Damu Salama Kanda ya Kati, lililopo Itega, Jijini Dodoma, akafafanua manufaa ya kutengenezwa mazao ya damu, kutasaidia kuokoa maisha ya wajawazito na wenye uhitaji.

Inatajwa kuwa, ni hali inayowapa wakati mgumu watoa huduma kliniki katika suala la wingi wa damu kwao, hata wahudumu wake wanafanya kazi ya ziada kuwanoa kwa elimu ya ziada, hivyo, kuwapo Mpango wa Mazao ya Damu Salama, mpango huo utasaidia ongezeko kubwa la damu nchini.

"Serikali imeongeza vituo saba vya kutengenezea mazao ya damu kama vile 'plasma', chembe sahani za damu na chembe hai nyekundu na kufanya kuwa na jumla ya vituo 15 nchi nzima kutoka vituo saba vya kanda, vilivyokuwa vikitengeneza mazao ya damu kwa mwaka 2021/2022."

Waziri Ummy anakiri licha ya kuwapo vituo, bado havikukidhi mahitaji. Ni wakati wizara kupitia Mpango wa Taifa wa Damu Salama, ilikukusanya mazao ya damu 25,658 aina ya Plasma (FFP), zinazotumika kusaidia kinamama wanaopata matatizo kutokwa na damu nyingi wakati wa kujifungua.

Vilevile Ummy anadems, jumla ya chupa 6,625 za chembe sahani (platelets) zimetumika kutibu wagonjwa wa saratani, seli mundu na waliokuwa na matatizo mengine wakati huo.

Waziri anafafanua kwamba hadi sasa katika harakati za kuuokoa majeruhi wa ajali, wajawazito, jamii imekuwa ikihamasika kuchangia damu, kwa lengo la kuhakikisha panakuwapo akiba ya damu inayotosha.

Ummy anasema, takwimu za ukusanyaji damu zinaonyesha mafanikio ya kuongozeka akiba ya damu inayokusanywa kila mwaka, akifafanua: "Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Mpango umeweza kukusanya chupa za damu 495,600 sawa na asilimia 84 ya mahitaji ya damu nchini, ikilinganishwa na chupa 366,206 zilizokusanywa mwaka 2021/2022 sawa na asilimia 67 ya mahitaji."

Kuhusu ufunguzi wa kituo cha Mpango wa Taifa wa Damu Salama Kanda ya Kati Dodoma, Waziri Ummy anasema, kitasaidia kuboresha huduma za damu salama kwa mikoa Kanda ya Kati, Iringa, Singida na Dodoma kwa kuzalisha mazao ya damu kwa ajili ya wahitaji.

**NAIBU KATIBU MKUU**

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dk. Grace Magembe, anasema kati ya Mei 2022 na Julai mwaka huu kuna vituo 43 vilivyotakiwa kutengeneza mazao ya damu salama, kati yao vituo 12 vimeshaanza kutengenezwa katika hospitali zote kitaifa, pia za kanda; Hospitali za Rufani za Geita, Iringa na Simiyu.

Anaeleza hali ya vituo vya upasuaji wa dharura hasa za kumtoa mtoto tumboni, anabainisha kwamba hadi sasa viko 500 kitaifa.



## HABARI DODOMA

## Nape aipongeza Vodacom usambazaji mawasiliano

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye amepongeza jitihada za Kampuni ya Vodacom Tanzania kwa kuunga mkono juhudi za serikali kuhamishia sehemu ya shughuli zake jijini Dodoma na kusambaza huduma za mawasiliano na kiteknolojia nchini.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa ofisi hiyo jana, Nape alipongeza jitihada hizo zikiwa zinalenga kuwasogezea Watanzania huduma bora na za uhakika popote walipo kama serikali inavyofanya kuhamishia baadhi ya shughuli zake katika makao makuu ya nchi ili kuwapunguzia usumbufu wa kusafiri umbali mrefu mpaka jijini Dar es Salaam.

"Kwa kipindi kifupi sekta yetu imeshuhudia mafanikio makubwa yakujivunia ambayo ni mchango mkubwa katika maendeleo yetu. Mafanikio hayo ni pamoja na ongezeko kubwa la idadi ya watumiaji wa simu kutoka laini zilizosajiliwa milioni 51.3 mwaka 2020 hadi kufikia watumiaji milioni 61.88 Machi, 2023 ambapo kati ya hao asilimia 30 wanamilikiwa na Vodacom."

"Katika kipindi hicho watumiaji wa intaneti wameongezeka kutoka watumiaji milioni 26 hadi milioni 33.1. Fanikio lingine ni kwa upande wa uchumi jumuishi ambapo kwa sasa watumiaji wa huduma za huduma za kifedha hapa nchini wameongezeka hadi kufikia wateja milioni 44.4, kwamba kati ya hao asilimia 36 wanamilikiwa na Vodacom kupitia M-PESA," alisema Nape.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom Tanzania PLC, Philip Besiimire, alisema wamefungua ofisi mpya ya kisasa katika makao ya nchi mkoani Dodoma, kuwahudumia wateja na wageni mbalimbali wa ndani na kimataifa wanaofika kwa shughuli binafsi na za kiserikali.

"Pia, tumezingatia suala la usawa na ujumuishi kwa wateja wetu wote hususani wenye ulemavu. Ofisi hii ina uwezo wa kuwahudumia wasiosikia au viziwi kwa alama za vidole na kutokuona au vipofu kupitia 'SAUTI PASS' inayomwezesha kutumia sauti yake kupata huduma," alisema na kuongeza:

"Lengo kubwa ni kuwajali wateja wetu na kuwapatia fursa ya kufurahia mawasiliano na kujiunga kidijitali, hii ni kuendana na dhamira yetu ya kuwa wabunifu kwa kuwapatia ufumbuzi katika kuwasiliana na kuzifikia huduma zetu," alisema Besiimire.

# Aweso: Bado lipo tatizo miradi ya maji kutokuwa endelevu

**Paul Mabeja na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amesema licha ya serikali kutumia fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya maji katika maeneo mengi nchini bado lipo tatizo la miradi hiyo kushindwa kuwa endelevu.

Aweso aliyasema hayo jana jijini hapa, wakati wa hafla ya uzinduzi wa bodi za wakurugenzi za mfuko wa maji taifa na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira vijijini.

Alisema ujenzi wa miradi ya maji hivi sasa siyo tatizo kwa kuwa serikali imekuwa ikiwezesha fedha nyingi katika maeneo mengi lakini tatizo lililopo hivi sasa ni kushindwa kuwa endelevu.

"Kujenga miradi ya maji sasa hivi RUWASA siyo tatizo tena mnaweza kujenga miradi mikubwa sana lakini kuwa endelevu ndiyo shida unakuta serikali imetoa Sh. bilioni nne, kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa maji lakini ukiharibika hata kubadili koki tuu inakuwa shida," alisema Aweso.

Aidha, Aweso aliitaka Bodi ya Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini kuangalia namna ya miradi ya maji inavyoweza kujiendesha yenyewe katika maeneo ya vijijini.

"Fedha za miradi ya maji zisiachiwe jumuiya lazima kuwapo na usimamizi, lazima sasa tujipime kama kuna haja ya kuendelea na mfumo huu wa kutumia jumuiya kuendesha miradi ya maji vijijini kuna muda nilienda kule Lupeta wilayani Mpwapwa mwenyekiti wa jumuiya kakimbia na fedha mhasibu hajui kitu," alisema.

Aweso pia aliiagiza Bodi ya Mfuko wa Maji wa Taifa kutafuta vyanzo vingine vya mapato badala ya kuendelea kutegemea fedha zinazotolewa na serikali.

"Serikali inatupatia fedha za mfuko wa maji kila mwezi lakini bodi hatupaswi kuendelea kutegemea chanzo kimoja kwani mahitaji bado mengi, hivyo tutafute namna nyingine ya kupata fedha, mbona kuna taasisi zinapata fedha na sisi tutafute vyanzo vingine vya mapato," alisema Aweso.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijimi (RUWASA) Bwai Biseko, alisema hadi kufikia Desemba 2022 miradi 2,273 ya miundombinu ilikuwa imejengwa na kukamilika kupitia fedha za ndani na wadau wa maendeleo.

"Miradi hiyo inanufaisha wananchi 11,641,230 katika vijiji 4,809. Katika kipindi hicho ujenzi wa mabwawa saba ulikamilika na jumla ya visima 947 vilichimbwa," alisema.

Alisema katika kipindi cha kuanzia Julai 2019 hadi Septemba 2022, RUWASA ilifanikiwa kuunda na kusajili CBWSOs 2,524 na zimeweza kuajiri wataalamu 5,586 wa fani za ufundi, uhasibu na kada saidizi ili kuwa na uendelevu wa huduma.



Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye (wa pili kulia), akizungumza na viongozi wa Vodacom Tanzania wakati wa uzinduzi wa ofisi mpya ya kisasa ya kampuni hiyo, yenye uwezo wa kuhudumia wasioona na kusikia pamoja na chumba maalum cha wajawazito na waliojifungua jijini Dodoma juzi. Wengine ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Selemani Kakoso (kulia), Mkurugenzi wa Kitengo cha Biashara, Linda Riwa (wa pili kushoto), Mkuu wa Kanda ya Kati, Joseph Sayi na Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom Tanzania, Philip Besiimire (wa nne kushoto nyuma). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kanisa lakemea tabia wazazi kuruhusu watoto kupara samaki

**Na Peter Mkwavila,** BAHI

MRATIBU wa Mradi wa Elimu Jumuishi unaosimamiwa na Kanisa la FPCT, Jann Mgidange, amewataka wazazi na walezi wa Kijiji cha Nagulo Wilaya ya Bahi mkoani Dodoma kuacha kuwaruhusu watoto wao wanaosoma kwenda kufanya kazi za kupara samaki kwa kuwa wanahatarisha mahudhurio yao shuleni.

Mgidange aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na wazazi na walezi wa kijiji hiko kwenye mkutano wa kijamii juu ya uhamasishaji wa masuala ya kielimu.

Aliwataka kuhakikisha wanafunzi hao wanasoma na hawajihusishi na kazi ya ajira ya kupaa samaki.

Alisema kuwa baadhi ya wazazi na walezi wa kijiji hicho wameamua kuwatumikisha watoto wao kwa kuwapeleka bwawani huko ili wakafanye kazi za kupaa samaki, huku wakitambua kuwa kwa kufanya hivyo ni makosa na wanawanyima haki ya kupata elimu ambayo itakayowasaidia wao wenyewe.

"Ninachukizwa na kitendo hiki cha mzazi au mlezi anamruhusu mtoto wake kwenda bwawani akafanye kazi ya kuparua samaki, wakati mkifahamu kuwa hilo ni kosa kubwa kwa kuwa linamnyima haki ya msingi ya mtoto huyo ya kupata elimu ambayo itakayomsaidia yeye mwenyewe na hata kwa familia husika," alisema.

Alisema kuwa watoto hao hivi sasa baadhi yao hawaendi shuleni badala yake wanajishughulisha na kazi mbalimbali zinazopatikana kwenye bwawa hilo la samaki ili kujipatia ujira wa fedha zitakazowawezesha kujiinua kiuchumi.

Maria Mathias, Julias Muhema ambao walijitambulisha ni wanafunzi walisema kuwa wanalazimika kufanya vibarua kwenye bwawa hilo ili kujipatia fedha zitakazokwamua kiuchumi kutokana na hali duni zilizopo kwenye familia wanazotoka.

Diwani wa Kata ya Bahi, Augustini Ndonu aliwataka wazazi na walezi kuhakikisha watoto wote wanaofanya kazi mbalimbali kwenye bwawa hilo wanashiriki kikamilifu kwenye kuhudhurio masomo na watakaobainika watachukuliwa hatua za kisheria.





# TFS yawatoa hofu wakazi Kata ya Nsala, Ruiwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKALA wa Huduma za Misitu nchini (TFS), umesema hauna lengo la kuwahamisha wananchi wa Kata ya Nsalaga iliyopo jijini Mbeya na Ruiwa iliyopo wilayani Mbarali kwenye makazi yao kama ambavyo walitoa malalamiko hivi karibuni.

Hivi karibuni wananchi wa kata hizo ambazo ziko kwenye maeneo yanayozunguka msitu huo, walilalamika kwamba wakala huo umevamia maeneo yao na kuweka mipaka mipya ya shamba la miti la Kawetere.

Akizungumza na wananchi hao wakati wa mkutano maalumu wa kutoa elimu ya uhifadhi wa mazingira, Mhifadhi Mkuu wa Shamba la Miti la Kawetere, Arnold Shoo, alisema lengo la wakala huo ni kuhakikisha msitu huo unakuwa salama.

Alisema hawajawahi kuwa na lengo la kuwaondoa wananchi hao kwenye maeneo yao ya makazi bali ni kuwazuia wasivuke mipaka na kuuharibu msitu ambao ni muhimu kwa mazingira na vyanzo vya maji.

Alisema kwenye mpaka kati ya maeneo ya wananchi na msitu huo kuna mawe ambayo wananchi hawatakiwi kuvuka na kwenda kufanya shughuli zao ndani ya msitu.

"Tumekuja hapa kwa lengo la kuwaambia kwamba mkishavuna mazao yenu kule msirudi tena kwenda kufanya shughuli yoyote, rudini huku na muendelee kufurahia maji yanayotoka kwenye msitu huu," alisema Shoo. Alisema wananchi hawataruhusiwa tena kulima wala kuingia na zana za aina yoyote kwenye msitu huo kwa maelezo kuwa wanahatarisha ustawi wake.

Alisisitiza kuwa msitu huo ni muhimu kwa vizazi vya sasa na vijavyo hasa kuhakikisha mazingira yanakuwa salama na hata vyanzo vya maji vilivyopo vinatunzwa.

Ofisa Misitu TFS, Isdory Chuwa, aliwataka wananchi wa maeneo yote yanayozunguka msitu huo kushirikiana na maofisa wa TFS kuulinda ili usitoweke kwa maelezo kuwa una umuhimu mkubwa.

Alisema kwa sasa walichokifanya ni kusafisha mpaka kati ya maeneo ya wananchi na msitu huo ili kuzuia moto unaoweza kuzuka kutoka kwenye mashamba ya wananchi kuvamia msitu na kuuteketeza.

Aliwataka wananchi kuhakikisha hawaanzishi moto ovyo kwenye maeneo hayo ili kuepuka kuuharibu msitu huo ambao alisema ni muhimu kwa maisha ya viumbe hai pamoja na uoto wa eneo hilo.

Alisema msitu huo umekuwa na faida mbalimbali kwa wananchi wa maeneo hayo ikiwamo kusaidia ujenzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo kama shule na zahanati.

"Sasa hivi mnanufaika na msitu huu kwa sababu kuna watu waliuhifadhi vizuri, kwa hiyo naomba nanyi tushirikiane kuhakikisha tunautunza msitu huu kwa faida ya vizazi vya baadaye," alisema Chuwa.

Baadhi ya wananchi wa maeneo hayo waliwashukuru maofisa wa TFS kwa elimu waliyoitoa wakidai kuwa itasaidia kuondoa mgogoro baina yao na msitu huo wa Kawetere.

Mmoja wa wananchi hao, Moses Kimbesa alisema baada ya kupatiwa elimu wako tayari kuacha kufanya shughuli zozote ambazo zinahatarisha msitu huo ikiwa ni pamoja na kuzuia moto.

Aliwaomba maofisa hao kuendelea kutoa elimu ya mara kwa mara kwa wananchi hao ili na wao washiriki kwenye utunzaji wa msitu huo pamoja na maeneo mengine ya misitu.

Msitu wa Kawetere una ukubwa wa zaidi ya hekta 3840 na unapakana na Halmashauri nne za Mkoa wa Mbeya ambazo ni Jiji la Mbeya, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Mbarali na Chunya.



Baadhi ya wamiliki wa mabasi na malori wa mikoa ya Mbeya, Njombe na Songwe, wakishiriki kikao cha wadau wa usafirishaji kilichoitishwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu (LATRA) jijini Mbeya juzi, kwa lengo la kusikiliza kero mbalimbali. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Ukosefu elimu ya mitaji, uwekezaji chanzo biashara kukua

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

IMEELEZWA kuwa uelewa mdogo wa wafanyabiashara wadogo kuhusu masoko ya mitaji na uwekezaji ndicho chanzo cha biashara zao kushindwa kukua na hivyo uchumi wao kudumaa.

Mkurugenzi wa Sera, Utafiti na Mipango wa Mamlaka ya Masoko ya mitaji na Dhamana (CMSA), Alfred Mkumbo, aliyasema hayo jana wakati wa mafunzo maalumu kwa wafanyabiashara mkoani Mbeya kuhusu shughuli hizo.

Alisema wafanyabiashara wengi hawana uelewa kuhusu namna ya kuyatumia masoko ya mitaji hasa kutoa dhamana kwa ajili ya wawekezaji kuwekeza fedha zao.

Vilevile alisema wawekezaji hawana uelewa wa kutosha kuhusu kuwekeza kwenye bidhaa za masoko ya mitaji kama vile hati fungani, hisa ama vipande vya uwekezaji wa pamoja. "Hili ni tatizo kubwa lakini kwa sasa tunaendelea na jitihada mbalimbali za kuhakikisha tunawajengea uelewa wananchi ili wawe wanawekeza fedha zao kwenye maeneo yote haya," alisema Mkumbo.

Alisema walianza kutoa elimu hiyo katika Mkoa wa Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza, Arusha, Zanzibar na kwamba Mkoa wa Mbeya ni wa sita na wataendelea katika mikoa mingine nchini.

Akifungua mafunzo hayo, Katibu Tawala Msaidizi wa Mkoa wa Mbeya anayeshughulikia rasilimali watu, Donald Bombo aliishukuru taasisi hiyo kwa kutoa elimu hiyo kwa wananchi akidai kuwa itasaidia kuboresha biashara.

Alisema zaidi ya asilimia 90 ya Watanzania hawana uelewa kuhusu masuala ya masoko hali ambayo inawafanya wasiwe na ufanisi wa kutosha kwenye biashara zao.

Alisema wafanyabiashara wengi wamekuwa wakiwekeza kwenye vyombo vya usafiri, nyumba za kuishi, kwenye kilimo na shughuli zingine ndogo jambo ambalo wakati mwingine linaweza lisiwe na tija.

"Elimu hii sasa itasaidia kuwahamasisha wananchi kuwekeza kwenye masoko ya mitaji, tutaachana na huu uwekezaji wa asili ambao hautusaidii sana," alisema Bombo.

Baadhi ya wafanyabiashara walioshiriki kwenye mafunzo hayo walisema elimu hiyo itawasaidia kuboresha biashara zao kwa kuboresha uwekezaji kwenye maeneo tofauti na yale ya asili ambayo walikuwa wakiwekeza.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Rose Leonard alisema elimu waliyoipata iliwasaidia kupanua uelewa wa uwekezaji kwenye masoko ya mitaji ambayo hawajawahi kuipata.

Alisema elimu hiyo ni muhimu kwao hasa katika kipindi hiki ambacho teknolojia imekuwa kubwa ikilinganishwa na miaka ya nyuma.

Naye Damas Madembwe alisema wafanyabiashara wamekuwa wakifanya shughuli zao lakini wanashindwa kuwakaribisha wawekezaji kutokana na elimu kuwa ndogo.

## TARI yaanza utafiti wa mahindi lishe kuondoa udumavu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) Kituo cha Uyole jijini Mbeya, imeanza kufanya utafiti wa mahindi lishe (mahindi ya njano) ili kusaidia wananchi wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kukabiliana na udumavu.

Mtafiti wa mahindi katika kituo hicho, Leonald Sabula, aliyasema hayo jana alipozungumza na Nipashe kuhusu shughuli mbalimbali zinazofanywa na taasisi hiyo hasa utafiti wa mbegu za mazao.

Alisema walianza kufanya utafiti huo mwaka juzi na wanatarajia kutoa matokeo ya awali mwaka huu baada hasa katika kipindi cha maonyesho ya wakulima (Nanenane).

Alisema wanakusudia kukamilisha utafiti huo mwakani na kuanza kusambaza mbegu hizo kwa wakulima ili zianze kulimwa kwenye maeneo ambayo watabaini kuwa yanafaa kuzalishwa.

"Kwa sasa tunapambana zaidi na tatizo la udumavu hasa kwa watoto, haya mahindi yamebainika kuwa yana virutubisho vingi ambavyo vinafaa kwa watoto kwenye mikoa yetu hii," alisema Sabula.

Sabula alisema mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini inazalisha chakula kwa wingi lakini ndiyo inayokabiliwa na udumavu kwa kiwango kikubwa.

Alisema mbali na mahindi hayo, pia kituo hicho kinazalisha mazao mengine yenye virutubishi muhimu kwa watoto ikiwamo viazi lishe na maharage.

Alisema mazao hayo yote yanatakiwa kuliwa na watu wote bila kujali umri huku akisisitiza kuwa ni muhimu zaidi kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano.

Hata hivyo Sabula alisema mahindi hayo yana soko kubwa duniani ambalo Watanzania wanatakiwa kuchangamkia kuzalisha hasa katika nchi ya Misri.

Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini inaongoza kwa uzalishaji wa chakula na inajulikana kama ghala la taifa la chakula lakini inaongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya watoto wenye udumavu.





## Naibu Waziri ataja faida ya takwimu kimaendeleo

**Na Mwandishi wetu,** ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Fedha na Mipango, Ali Suleiman Ameir, amesema uwepo wa mkakati wa kuendeleza takwimu Zanzibar, utasaidia kuongeza uzalishaji na utumiaji wa takwimu wakati wa kupanga mipango ya maendeleo.

Aliyasema hayo visiwani Zanzibar wakati wa uzinduzi wa mkakati wa kuendeleza takwimu Zanzibar, kueleza kuwa maendeleo ya Zanzibar yanahitaji takwimu sahihi na utayarishaji wa mkakati ambao utasaidia mahitaji makubwa ya takwimu kwa ajili ya kufuatilia na kutathmini mipango ya maendeleo.

Alisema mahitaji ya takwimu yanazidi kuongezeka kadri nchi inavyopiga hatua za maendeleo, hivyo upatikanaji wa takwimu hizo unategemea kwa kiasi kikubwa uwezo wa taasisi katika uzalishaji.

Alisema rasilimali kubwa za watu na fedha zinawekezwa katika ukusanyaji wa taarifa za takwimu, lakini, bado kuna changamoto ya kukidhi haja ya mahitaji kulingana na uwezo wa taasisi wa kukusanya, kuchambua na kusambaza.

Alisema umuhimu huo umeleta msukumo mpya kwa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali katika kutoa takwimu sahihi zinazozingatia wingi, wakati na ubora.

Hata hivyo, alisema mfumo wa takwimu wa Zanzibar umeonekana kuwa na uwezo mdogo kutokana na ukosefu wa mkakati, udhaifu wa miundo ya kitaasisi pamoja na uratibu wa upatikanaji wa takwimu kwa wadau mbalimbali.

Alisema ili Zanzibar kuwa na maendeleo endelevu, mahitaji ya takwimu bora kwa muda sahihi ni muhimu kwa ajili ya kufuatilia utekelezaji wa Malengo ya Dira ya Maelendeo ya Mwaka 2050, Sera ya Uchumi wa Buluu.

Pia ni muhimu katika Mpango wa Maendeleo ya Zanzibar (ZADEP) pamoja na mipango ya kisekta na utekelezaji wa mikakati ya kidunia kama vile Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), Agenda ya Maendeleo ya Afrika 2063, Dira ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2050 pamoja na mipango mengine ya maendeleo.

Alisema mkakati wa kuimarisha takwimu Zanzibar utakuwa ni muundo wa kujenga uwezo wa kitakwimu na kutengeneza mfumo utakaoimarisha uzalishaji wa takwimu na matumizi yake.

Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Salum Kassim Ali, alisema, takwimu bora na za uhakika zinazopatikana kwa wakati huwezesha upimaji, ufuatiliaji na usimamizi bora wa matokeo ya kile ambacho serikali, washirika wa maendeleo, sekta binafsi na umma hutekeleza katika kuimarisha ustawi wao.

Mwakilishi wa UNFPA, Mark Bryan Schreiner, alisema mkakati huo utaongoza juhudi za kukusanya, kuchambua, na kusambaza taarifa sahihi za takwimu kwa wakati.

# UNFPA yakabidhi gari kusaidia huduma za afya mama, mtoto

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA) limekabidhi gari kwa Wizara ya Afya lenye thamani ya Sh. milioni 85 kwa ajili ya kuboresha masuala ya ufuatiliaji wa huduma za afya za mama na mtoto.

Akizungumza visiwani Zanzibar katika hafla ya makabidhiano ya gari hiyo, Mwakilishi wa shirika hilo Tanzania, Mark Bryan Schreiner, alisema vifo vya wajawazito visiwani Zanzibar vimeendelea kutia hofu na masuala ya afya ya uzazi kuwa miongoni mwa chanzo kikuu cha vifo hivyo.

Alisema matumizi ya uzazi wa mpango ambayo yanakubalika katika kupunguza vifo vya uzazi bado ni chini ya asilimia 14 na mahitaji ambayo hayajafikiwa ni kati ya juu zaidi ya asilimia 28.

Schreiner alisema kwa miaka mingi UNFPA imekuwa ikisaidia Wizara ya Afya kuimarisha utoaji wa huduma bora za afya ya uzazi.

Aidha, alisema msaada huo unaenda sambamba na mafunzo ya watoa huduma za afya, usimamizi shirikishi kwa halmashauri za wilaya, afya za jamii na shughuli nyingine za kuzalisha mahitaji.

"Madhumuni ya gari hili liliombwa na Wizara ya Afya na kununuliwa na UNFPA ni kusaidia uratibu wa afya ya uzazi Zanzibar ambazo ni pamoja na usimamizi wa usaidizi, ufuatiliaji na ukuzaji uwezo,"alisema.

Gari hili litaongeza kasi ya juhudi za kutoa huduma bora za afya ya uzazi kwa wote na kuchangia ustawi wa familia na jamii.

Hata hivyo alisema makabidhiano ya gari hilo ni juhudi za UNFPA zinazoendelea na dhamira ya kuwezesha uratibu wa afya ili kuhakikisha kuwa wanawake na vijana wanapata huduma zinazohitajika ili kuokoa maisha yao.

Naye Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, alisema huduma za afya ya uzazi wa mpango zinasaidia kupunguza vifo vya mama na watoto na kustawisha afya zao.

Mazrui, alilipongeza UNFPA kwa misaada yao katika kuboresha huduma za afya za uzazi hasa katika kuhakikisha vifo vya mama na mtoto vinapungua.

Aidha, alisema licha ya juhudi za washirika wa maendeleo na serikali lakini bado nguvu za ziada zinahitajika katika kuokoa maisha ya mama na mtoto.

Kwa mujibu wa taarifa za Wizara ya Afya Zanzibar, idadi ya wanawake wanaofariki katika vituo vya afya kutokana na matatizo ya uzazi imepungua kutoka 70 mwaka 2021 hadi 53 mwaka 2022 na vifo vya watoto wachanga kutoka 542 mwaka 2021 hadi 421 mwaka 2022.




Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, akionyesha kitabu chenye mapendekezo ya wadau baada ya kufunga mradi wa "Amani Yetu Mshikamano Wetu", Zanzibar juzi. Mradi huo, uliofadhiliwa na Jumiya ya Ulaya (EU), uliendeshwa kwa zaidi ya mwaka mmoja na nusu kutekelezwa kwa ushirikiano kati ya Shirika la Konrad Adenauer Stifftung (KAS) la Ujerumani na Jumuiya ya wanasheria wanawake Zanzibar. **PICHA: OFISI YA MKRZ**

# Makamu wa Rais ataja chanzo migogoro ya kisiasa Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Othman Masoud Othman amesema jamii ya Zanzibar imeathiriwa na migogoro ya kisiasa inayotokana na uchaguzi.

Alisema matokeo mabaya ya migogoro hiyo ndio husukuma uwepo wa miradi ya kuhamasisha amani na utengamano wa kijamii. Aliyasema hayo visiwani Zanzibar katika hafla ya ufungaji wa mradi wa 'amani yetu, mshikamano wetu' ambapo hafla hiyo iliwakutanisha washiriki mbalimbali ikiwemo viongozi wa vyama vya siasa, dini, serikali na asasi za kiraia.

Othman alisema haikuwa rahisi Zanzibar kukuta viongozi wa kisiasa kutoka vyama mbalimbali wakijumuika kwa pamoja katika mijadala au vikao hata hile vyenye maslahi ya kijamii.

Alisema hali hiyo ilitokana na chuki, kutoaminiana na uhasama mkubwa uliokuwepo miongoni mwa wanasiasa kutokana na kuhitilafiana katika uungaji mkono wa vyama vya siasa.

"Hali hiyo ilitufikisha pahala pabaya sana, si vyema kuyakumbusha yaliyopita lakini ni muhimu kuyazingatia na kuyatafakari kwa makini,"alisema Othman.

Aidha, alisema kwa jitihada za pamoja na wadau mbalimbali imefikia pahala imeanza kuonekana Zanzibar yenye fursa ya kupiga hatua ya kujenga misingi endelevu ya amani na mshikamano.

Alisema maelewano ya watu katika nchi hufungua milango ya neema na baraka kwa sababu amani na utulivu vinaimarika na shughuli za kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Hata hivyo alisema lengo kuu la mradi huo ni kuchangia usuluhishi wa migogoro ya kisiasa na ustawi wa amani, hivyo lazima kuwe na mifumo madhubuti inayosaidia utatuzi wa migogoro.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, alisema bado kunasafari ndefu hivyo ni vyema kujipanga vizuri katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi mkuu ili kudumisha amani.

Alisema yeye ni muumini wa maridhiano ya kisiasa na tangu ilipoundwa serikali hiyo yumo katika Baraza la Mawaziri hivyo anajua umuhimu wake.

Viongizi wa vyama vya siasa walioshirika katika hafla hiyo, walisema mradi huo umesaidia katika kudumisha amani ya nchi na kujenga uvumilivu wa kisiasa kwa wananchi.

Naibu Katibu Mkuu wa CHADEMA Zanzibar, Salum Mwalimu, alisema: "Amani ni tunda la haki. Pasipo na haki hakuna amani tutaendeleo kudanganyana, hivyo tustawishe haki na hicho ndicho CHADEMA tunachokiamini".

Mratib wa mradi huo, Almas Muhamed alisema tathmini ya mradi huo inadhihirisha kuwepo kwa mabadiliko chanya ikiwamo kuongezeka kwa uwaminifu kati ya watendaji wa kisiasa na wananchi, ushirikiano katika jamii na kuwa kitu kimoja na kujenga jamii isiyo chuki na migogoro ya kisasa.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

3FORM 58
IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE
AT ONE STOP CENTRE
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 671 OF 2023
In the Matter of the Estate of the Late
LILIAN ERICK JULIUS
And
In the matter of Application for letters of administration by
MICHAEL ERICK JULIUS

GENERAL CITATION
( Rule 75)

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above-named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 02 day of AUGUST 2023.

Dated at DAR ES SALAAM this 23 day of JUNE 2023

Senior Resident Magistrate

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA MBEYA
KITUO CHA MJINI MKOA WA MBEYA
SHAURI LA MADAI 134/2023
JINA LA MDAI BERNAD YOBELE NSELUA
JINA LA MDAIWA ELIAS KOMBA
KUITWA SHAURINI MDAIWA
(kanuni ya 10 ya kanuni za utaratibu wa Madai katika Mahakama za Mwanzo)

**KWA: ELIAS KOMBA\Kwa kuwa Mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba (eleza hapa habari za madai)**

**MADAI YA PESA TSH MILIONI TANO NA LAKI TANO TU (5500000/=)**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 30 mwezi 6 mwaka 2023 saa 08:30 asubuhi/mchana kwa mujibu wa madai haya na kwa kuwa siku hiyo ya kusikilizwa shauri hili na lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea.

HAKIMU
HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
MJINI

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya MASWA.
Kituo cha NYALIKUNGU mkoa wa SIMIYU
Usimamizi wa Mirathi Na.17/2023
KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU PAGALASI CHARLES LUPIA WA ISULILO-MASWA.
KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA GEORGE CHARLES LUPIA

**TANGAZO**

***(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)***

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 17 Mwezi 7 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia:**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuleta mahakamani kukaguliwa.
*Marehemu hakuacha wosia
Imetolewa leo tarehe **26 Mwezi 6 Mwaka 2023.**

MAHAKAMA YA MWANZO NYALIKUNGU MASWA

**Hakimu**
**HAKIMU MKAZI**
**MAHAKAMA YA MWANZO NYALIKUNGU.**

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**GYLEN SYLVESTER NGUBI** anatangaza kupotelewa na Cheti chake cha Chuo Kikuu pamoja na Nakala ya Matokeo vyote vikiwa na Namba ya usajili **BAED 70384/2021** vyenye majina ya usajili tajwa hapo juu Mali ya Chuo Kikuu cha SAUT. Mtu yeyote atakaye vipata awasiliane kwa namba **0674607598**
**RB: DSM/PHQ/RB/39157/2023**

---

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**JONATHAN PATRIC MCHARO** anatangaza kupotea kwa hati ya kusafiria yenye namba **:TAE 164670** iliyotolewa makao makuu **PCO DAR ES SALAAM** mwaka **2019.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: DAR/URA/214486/2023**

---


## KUPOTEA KWA CHETI



**GYLEN SYLVESTER NGUBI** anatangaza kupotelewa na Cheti chake cha Chuo Kikuu pamoja na Nakala ya Matokeo vyote vikiwa na Namba ya usajili **BAED 70384/2021** vyenye majina ya usajili tajwa hapo juu Mali ya Chuo Kikuu cha SAUT. Mtu yeyote atakaye vipata awasiliane kwa namba **0674607598**
**RB: DSM/PHQ/RB/39157/2023**


---

**SPECIAL POWER OF ATTORNEY**
**Know all Men whom it may concern**

BY THIS DEED,I, ROSEMARY MASHIMBA , the administratix of the estate of the late MASASI JOHN of P.O.BOX 139 GEITA(Here in after known as the donor) DO HERE BY APPOINT JOHN MASASI JOHN of P.O.BOX 139 GEITA, who is my son and he is living for gain in Geita, to be my attorney and to act as my attorney in respect of changing the names of Primary mining licenses owned by my late husband MASASI JOHN into my names due to the reasons that I am very sick.

That, the said ATTORNEY, shall have full power and authority to represent me and where necessary to initiate any legal process, or negotiations related there to accept the service of and to appear or represent me in Mining office or before any other office/officer whatsoever and for me and my name to commence, defend and conduct any action or other proceedings related to


- That shall present himself on my behalf to take charge and to deal with matters arising and pertaining to all processes of changing the names of Primary Mining licenses/ businesses licenses which were under the names of my late husband into my names.
  - That, he shall deal with the collection of all documents from the mining office and any other authority where require on my behalf.
  - That, he shall pay all fees, charges and outgoing whatsoever payable by me concerning mentioned case above.
  - That, he shall make and sign application and any other whatsoever on my behalf concerning businesses which were under the names of my late husband MASASI JOHN into my names.

AND GENERALLY, to execute and do all such deeds and things which the same shall deem it necessary or appropriate with the same effect as I had done, executed or performed it myself to the reason that I am very sick and I cannot perform this process.

This power of attorney is valid until the end of the process.

In witness where of I have hereunto set my hand this 28Th day of June, 2023 in this special power of attorney.

SIGNED and DELIVERED by the said ROSEMARY MASHIMBA ... DONOR



---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KATIKA MAHAKAMA KUU YA TA TANZANIA
DAR ES SALAAM
SHAURI LA MADAI NA. 235 YA 2022
TATA AFRICA HOLDING (T) LIMITED.......................MDAI
DHIDI YA
- MOHAMED SAID MOHAMED..................MDAIWA
- SAID MOHAMED ZAID.......................MDAIWA

1. **Mohamed Said Mohamed,**
   **P.O.Box 106 5**
   **Forest Mpya**
   **Jumbe Mtoto St**
   **Morogoro.**

2. **Said Mohamed Zad**
   **P.O.Box 1065**
   **Forest Mpya**
   **Jumbe Mtoto St**
   **Morogoro**

**KUITWA SHAURINI**
Kwa kuwa mdai aliyetajwa hapo juu, amefungua shauri la mdai dhidi yenu, shauri ambalo maelezo yake yameelezwa katika nakala ya hati ya madai inayopatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo mnatakiwa kuhudhuria katika Mahakam hii ninyi wenyewe au wakili au mwakilishi wenu anayeruhusiwa kisheria,siku ya tarehe 06/07/2023 saa tatu (3.30) kamili asubuhi mbele ya MHE,JAJI H.R.MWANGA kujibu madai dhidi yako .

Unaagizwa kuleta vielelezo vyote ambavyo unatarajia kuvitumia katika utetezi wako siku hiyo.

**ANGALIA**
Kama unapohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na mahakama ikithibitisha kuwa umepokea taarifa hii ya kuitwa shaurini, basi shauri inaweza kusikilizwa na kuamuliwa bila uwepo wako

HATI hiii imetolewa kwa AMRI yangu na CHAPA ya Mahakama leo hii tarehe 20/06/2023

DEPUTY REGISTRAR
DAR ES SALAAM ZONE

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya MOROGORO
Kituo cha MJINI
Mkoa wa MOROGORO
Usimamizi wa mirathi Na. 58/2023
KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU
AMINA RASHIDI SALUM MDOGWA WA MANGO
KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA AMIRI JUMA KONJA

**TANGAZO**

**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe **03** Mwezi **07** mwaka **2023** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia:** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa

* Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani na waweza kukaguliwa
* Marehemu hakuacha wosia *Futa isiyohusika

Imetolewa leo tarehe 27 mwezi 06 mwaka 2023

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya MOROGORO
Kituo cha MJINI
Mkoa wa MOROGORO
Usimamizi wa mirathi Na. 59/2023
KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU
SILVESTER SIMON NJIGU wa SULTAN AREA
KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA IRMINA SILVESTER SIMON

**TANGAZO**

**(kanuni ya 5 (2) ya kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe **03** Mwezi **07** mwaka **2023** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia:** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa

* Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani na waweza kukaguliwa
* Marehemu hakuacha wosia *Futa isiyohusika

Imetolewa leo tarehe 28 mwezi 06 mwaka 2023

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

---


**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 0677020701**
**E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,**
**WEBSITE: WWW.IPPMEDIA.COM**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

## Sheria uhesabuji umri yarekebishwa Korea Kusini

**SEOUL,** Korea Kusini

RAIA wa Korea Kusini wamekuwa wachanga kwa mwaka mmoja au miwili huku sheria mpya ya taifa hilo ikipatanisha mbinu mbili za jadi za taifa za kuhesabu umri na viwango vya kimataifa.

Sheria hiyo inafutiliwa mbali mfumo mmoja wa kitamaduni uliowachukulia Wakorea Kusini kuwa na umri wa mwaka mmoja wakati wa kuzaliwa, baada ya kuhesabu muda wakiwa tumboni.

Utamaduni mwingine ulikuwa ukihesabu kila mtu kuwa anazeeka kwa mwaka kila siku ya kwanza ya mwezi Januari badala ya siku zao za kuzaliwa, huku ikibainishwa kwamba kuanza kuhesabu umri kulingana na tarehe ya kuzaliwa kulianza jana.

Rais wa taifa hilo, Yoon Suk-yeol (pichani chini) alishinikiza vikali mabadiliko hayo alipowania wadhifa huo mwaka jana, akieleza kwamba mbinu za jadi za kuhesabu umri zilisababisha gharama zisizo za lazima za kijamii na kiuchumi.

Aidha, inaelezwa kuwa nchini humo mizozo imeibuka kuhusu malipo ya bima na kuamua kustahiki kwa programu za usaidizi za serikali.

Hata hivyo, awali njia ya hesabu iliyotumiwa sana nchini Korea ilikuwa mfumo wa umri wa Korea wa karne nyingi, ambao mtu huwa na mwaka mmoja wakati wa kuzaliwa na kupata mwaka tarehe moja Januari.

Kwa mujibu wa utaratibu huo, hiyo ina maana mtoto aliyezaliwa tarehe 31 Desemba atakuwa na umri wa miaka miwili siku inayofuata.

Mfumo tofauti wa kuhesabu umri, ambao pia ulitumiwa wakati wa jadi nchini humo, unazingatia mtu kuwa hana miaka lakini anakuwa na mwaka mmoja anapofikisha tarehe moja Januari.

Ilielezwa kuwa kufikia tarehe 28 Juni mwaka huu, mtu aliyezaliwa Juni 29 atakuwa na umri wa miaka 19 chini ya mfumo wa kimataifa, miaka 20 chini ya mfumo wa kuhesabu umri, na 21 chini ya mfumo wa umri wa Korea.

Raia watatu kati ya wanne wa Korea Kusini pia waliunga mkono uwekaji viwango, kulingana na kura ya maoni ya kampuni ya ndani ya Hankook Research Januari 2022.



Ilibainishwa kuwa wabunge walipiga kura kufuta mbinu za jadi za kuhesabu kura Desemba 2022. **BBC**

# Ujerumani na Afrika Kusini kuimarisha ushirikiano

**PRETORIA,** Afrika Kusini

AFRIKA Kusini na Ujerumani zinakusudia kuimarisha ushirikiano wa pande mbili katika nyanja tofauti licha ya kuwa na misimamo inayotofautiana kuhusu uvamizi wa Russia nchini Ukraine.

> **Hilo liko mikononi mwa Rais wa Russia, sote duniani tunatamani amani na ndio maana amani ndio jambo muhimu zaidi kwetu.**

Baada ya Waziri wa Mambo ya Nje wa Ujerumani, Annalena Baerbock, kufanya ziara nchini Afrika Kusini alikutana na mwenzake katika taifa hilo, Naledi Pandor mjini Pretoria na kufanya mazungumzo ambayo kwa pamoja walisisitiza umuhimu wa uhusiano baina ya nchi hizo mbili.

Ilieleza kuwa ajenda zilizojitokeza ni pamoja na kuimarisha ushirikiano katika masuala ya uchumi, utalii, mapambano dhidi ya athari za mabadiliko ya tabianchi na janga la Covid-19.

Pia suala la vita vya Russia nchini Ukraine, lilitajwa kutawala mazungumzo ya mawaziri hao na kwamba katika mazungumzo hayo waziri Baerbock aliitaka Russia kuacha kuishambulia Ukraine.

Aidha, kuhusu tukio la uasi la hivi karibuni lililofanywa na kundi la mamluki la Wagner, waziri Baerbock alieleza kuwa Ujerumani haiingilii kati masuala ya Russia, huku akitahadharisha kwamba Ujerumani inafuatilia kwa karibu hali ya mambo ingawa msukumo wao unasalia kwa vita vya Ukraine.

"Na hali ilivyokuwa mwishoni mwa juma lililopita inadhihirisha kwa mara nyingine tena kwamba Putin pia anahatarisha usalama wa nchi yake kwa vita hivi ambavyo ni kinyume na sheria za kimataifa, na ndiyo maana wito wetu wa dharura ni kwamba vita hivi lazima viishe.

"Hilo liko mikononi mwa Rais wa Russia, sote duniani tunatamani amani na ndio maana amani ndio jambo muhimu zaidi kwetu," alisema Baerbock. **DW**



Waziri wa Mambo ya Nje wa Ujerumani, Annalena Baerbock, akisalimiana na Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa.
**PICHA: MTANDAO**

## Kanisa Katoliki lamkosoa Rais Felix Tshisekedi

**KINSHASA,** DRC

KANISA Katoliki nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, (DRC) limekosoa kauli aliyoitoa Rais Felix Tshisekedi kuwa kanisa hilo limekosa mwelekeo na kuwagawa wananchi kuhusu maandalizi ya uchaguzi wa mwezi Desemba mwaka huu.

Katibu Mkuu wa Baraza la Maaskofu nchini humo (CENCO), Donatien N'shole, alikanusha madai hayo na kusema kwamba kanisa hilo litaendelea kusimama na wananchi na kushirikiana na utawala uliopo.

"Tuchukulie mambo kwa mtazamo chanya, yeye ndiye mdhamini mkuu wa usalama wa taifa letu. Usalama lazima uwe kipaumbele chake kama hilo ndilo analojitolea kwao," alisema N'shole.

Kanisa Katoliki lenye ushawishi mkubwa kwenye siasa za DRC limeendelea kukosoa maandalizi ya Tume ya Uchaguzi ya nchini humo (CENI) na kutilia shaka, iwapo tume hiyo itasimamia uchaguzi huru na haki.

Rais wa DRC, Felix Tshisekedi, hivi karibuni akiwa huko Mbuji-Mayi, alionyesha kusikitishwa na kile alichosema mvutano wa ndani katika kanisa hilo nchini humo, baada ya mwishoni mwa juma kanisa hilo kukosoa mchakato wa uchaguzi.

Tshisekedi, alisema badala ya kuvutana, kanisa hilo lilipaswa kufanya kazi kwa karibu na serikali kuhakikisha nchi inakuwa na amani hasa wakati huu wanapoelekea kufanya uchaguzi mkuu.

Kauli yake aliitoa wakati wadau wa uchaguzi wakijaribu kuweka shinikizo kwa tume ya uchaguzi CENI kuandaa uchaguzi ulio huru, haki na kuaminika.

Aidha, Mwenyekiti wa Tume hiyo, Dénis Kadima, ametangaza utaratibu wa wagombea kuwasilisha maombi ya kuwania nyadhifa mbalimbali kuelekea uchaguzi huo. **RFI**

## Wanaowasaidia Wagner wanyooshewa kidole

**WASHINGTON,** Marekani

MAREKANI imelaumu baadhi ya kampuni kutoka Umoja wa Falme za Kiarabu UAE, Jamhuri ya Afrika ya Kati pamoja na serikali ya Russia kwa kujihusisha kwenye biashara haramu ya dhahabu ili kufadhili kundi la mamluki la Wagner.

Taarifa ya Wizara ya Fedha ya Marekani ilisema kwamba taifa hilo limeweka vikwazo kwa kampuni nne zinayohusishwa na Wagner pamoja na kiongozi wake Yevgeny Prigozhin, zikidaiwa kutumika kulipa vikosi vya kundi hilo vinavyopigana Ukraine, pamoja na kuongoza operesheni zinazozingatia maslahi ya Russia barani Afrika.

Brian Nelson ambaye ni Naibu Waziri wa Fedha wa Marekani kupitia taarifa hiyo alisema kwamba kundi la Wagner linafadhili operesheni zake kwa kuiba mali asili kwenye mataifa kama Jamhuri ya Afrika ya Kati pamoja na Mali. **VOA**

# SINGIDA FOUNTAIN GATE FC YAANZA MIKAKATI LIGI KUU

Na Shufaa Lyimo

BODI ya Wakurugenzi ya klabu ya Singida Fountain Gate FC imeanza mikakati kuelekea msimu mpya wa ligi kuu Tanzania Bara.

Bodi hiyo jana ilikutana kupitia ripoti ya kocha Hans van der Pluijm ambapo mbali na mambo mengine pia imejadili eneo la kuweka kambi timu hiyo kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Mseмaji wa timu hiyo Hussein Masanza alisema moja kati ya mambo ambayo yalijadaliwa ni pamoja na usajili wa maboresho kwenye timu hiyo.

> "Kesho (leo) kikao kitaendelea na baada ya kumalizika tutajua timu itaweka kambi wapi na kuweka wazi mikakati yetu kuelekea msimu mpya, lengo la bodi ni kuona timu inafanya vizuri zaidi msimu ujao," alisema Masanza.

Alisema wamepanga kufanya maboresho makubwa ndani ya kikosi hicho kwa kusajili wachezaji wenye viwango vya juu ili kuwapa burudani mashabiki wao.

"Pia tuna malengo ya kufanya vizuri kwenye mashindano ya kimataifa, usajili wetu pia utalenga maeneo hayo, mashabiki na wapenzi wa timu yetu wasubiri kuona mabadiliko makubwa ," alisema Masanza.

Aidha, alitaja maeneo ambayo yamependekezwa kufanyiwa maboresho kuwa ni safu ya ulinzi, Ushambuliaji, viungo wa pembeni na kati.

"Tunawachezaji wengi wazuri kwenye safu hizo lakini tunataka kuongeza nguvu zaidi ili tufanye vyema kwenye michuano ya Kimataifa," alisema Masanza.

Alisema wamepania kuhakikisha msimu ujao wanafanya vizuri na wana kikosi ubingwa basi washike nafasi za juu zitakazowapa nafasi ya kushirikimashindano ya kimataifa kama ilivyo msimu huu.



Vijana wanaolelewa katika Kituo cha kukuza vipaji cha Jakaya Kikwete, wakifanya mazoezi kwenye viwanja vya kituo hicho jana. **PICHA: JUMANNE JUMA.**

# Mbeya City yataja kilichoitafuna, yaahidi kurejea tena Ligi Kuu

Na Adam Fungamwango

KLABU ya Mbeya City imeahidi kurejea tena kwenye Ligi Kuu baada ya msimu ujao, huku ikianika mapungufu yaliyosababisha iteremke daraja.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) mkoani Mbeya, Ndele Mwaselela alisema timu hiyo haikufanya vizuri msimu huu kwa kukosa motisha, huku matatizo mengine yakifichwa badala ya kuwekwa hadharani ili yarekebishwe.

"Kusema kweli timu yetu ilikosa motisha na hamasa na waliosababisha hivyo ni sisi wenyewe watu wa Mbeya, wakiwemo Wanahabari, hawakuwa wanaeleza au kuandika na kuweka hadharani matatizo yanayoikumba klabu ili yatatuliwe, badala yake watu wakaona kila kitu kiko sawa tu, mnakuja kulaumu baada ya timu kushuka," alisema Mjumbe huyo.

Alishangaa kuona hamasa na motisha zinafanywa kuinusuru wakati timu ipo kwenye hali mbaya ya kucheza 'play off.'

"Kwa kweli tulikuwa tumeshachelewa, lakini hili sasa ni somo, tutakaa upya, lazima tuitengeneze vizuri kwa kufanya usajili bora ili rudi kwenye Ligi Kuu, naamini tutacheza Ligi ya Championship msimu huu na kurejea tena," alisema.

Mbeya City iilishuka daraja Jumamosi iliyopita ilipopata kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Mashujaa FC kutoka Kigoma kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya.

Hicho kilikuwa kipigo cha pili, kwani wiki moja iliyopita, Mbeya City ilikumbana na kipigo cha mabao 3-1 dhidi ya timu hiyo, Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma.

Timu hiyo inashuka daraja baada ya kucheza Ligi Kuu kwa miaka 10, tangu ilipopanda msimu wa 2013/14 na ikawa timu tishio kiasi cha kumaliza ikiwa nafasi ya tatu kwa pointi 49, mbele ya Azam ilikuwa bingwa na Yanga iliyoshika nafasi ya pili, ikiidondosha Simba hadi nafasi ya nne.

Msimu wa 2014/15 pia haikufanya vibaya kwani ilishika nafasi ya nne chini ya Yanga, Azam na Simba.

## TPBRC yatoa onyo waandaaji ngumi

Na Shufaa Lyimo

KAMISHENI ya ngumi za kulipwa nchini (TPBRC) imetoa onyo kali kwa waandaaji wa mapambano ya ngumi (mapromota) ambao wanaandaa mapambano bila kuwalipa mabondia stahiki zao.

Akizungumza na Nipashe Jijini Dar es Salaam jana, Rais wa Kamisheni hiyo Chaurembo Palasa alisema 'Promota' atakayebainika kutomlipa bondia atafungiwa pamoja na kutozwa faini.

"Promota hawezi kuchezesha pambano bila kumpa pesa bondia na akikiuka kanuni na taratibu atachukuliwa hatua, hii tunawakumbusha wale wote wanaoandaa mapambano ya ngumi kuhakikisha wanamalizana kwanza na mabondia," alisema Palasa.

Aidha alisema bondia ambaye atachukua pesa na kutopanda ulingoni malalamiko hayo yakiwafikia atampelekwa kamati ya nidhamu ambayo itampa adhabu ikiwa pamoja na kufungiwa kucheza ngumi ndani na nnje ya nchi.

Palasa alisema kwa sasa mabondia wengi wanalipwa fedha nyingi tofauti na miaka iliyopita na hii inatokana na mchezo huo kuanza kupata umaarufu mkubwa.

"Kwa sasa mchezo wa ngumi upo juu na ndio maana tunaona mabondia wengi miaka ya sasa wanafaidika kwa kiasi kikubwa kwani wanapomaliza mapambano wanalipwa kiasi kikubwa cha pesa tofauti na walivyokuwa wanalipwa miaka ya nyuma," alisema Rais Palasa.

## Korosho Queens yajivunia kiwango

Na Shufaa Lyimo

KOCHA wa timu ya Wavu ya Korosho Queens, Gabriel Joshua amesema kufanya vizuri kwenye mashindano ya Taifa ya mchezo huo yanayoendelea jijini Dar es Salaam kunatokana na kujituma na viwango bora vya wachezaji wake.

Gabriel alisema, licha ya ugumu wa michuano hiyo inayofanyika kwenye uwanja wa Gwambina, wachezaji wake wameonyesha ukomavu mkubwa kwa kujituma kuanzia mazoezini mpaka kwenye mechi.

"Wachezaji wangu wamefanya kazi kubwa, kwanza wanacheza na timu zenye wakongwe wengi, nashukuru wanafuata maelekeo yangu na ndio maana tunafanya vizuri," alisema Gabriel.

Timu hiyo kutoka Mkoani Mtwara juzi ilifanikiwa kuibuka na ushindi wa Seti 3-1 dhidi ya Mafinga Parish ya Iringa kwenye mchezo uliokuwa na upinzani mkubwa.

Akizungumzia matokeo hayo, mchezaji wa timu hiyo Vanesa John alisema ligi ya mwaka huu imekuwa ngumu na kila timu imejiandaa vizuri kuweza kushinda taji la michuano hiyo.

HABARI MICHEZO

ZISIKUPITE

### KANE AITAKA BAYERN

MSHAMBULIAJI wa Tottenham Hotspur, Harry Kane, 29, anataka kujiunga na Bayern Munich, lakini ofa ya ufunguzi ya klabu hiyo ya Ujerumani ya pauni milioni 60 pamoja na nyongeza kwa nahodha huyo wa England imeonekana kuwa ni ya chini sana na watahitaji kutoa angalau pauni milioni 100 ili kupata nafasi kukamilisha mpango huo. ***(Guardian)***

### RICE OFA YA TATU

ARSENAL imewasilisha ofa ya tatu kwa kiungo wa kati wa West Ham na England, Declan Rice, 24, huku ofa hiyo ikijumuisha pauni milioni 100 na nyongeza zaidi ya pauni milioni 5. ***(Subcsription)***

### DE GEA NA MAN

GOLIKIPA wa Hispania, David de Gea, 32, alitia saini mkataba wa kurefusha mkataba na Manchester United, lakini klabu hiyo ya Old Trafford iliunga mkono mpango huo na badala yake imempa mshahara mdogo kuliko ilivyokuwa awali. ***(Mail)***

### LIVER YAMTAKA MBAPPE

LIVERPOOL iko tayari kushindana na Real Madrid katika kujaribu kumsajili fowadi wa Paris St-Germain Mfaransa Kylian Mbappe, 24, kwa dau la zaidi ya euro milioni 300, kwa mujibu wa wakala wa Fifa, Marco Kirdemir. ***(Marca)***

### LUKAKU ATAKIWA

INTER Milan inajiandaa kuwasilisha ombi jipya la kumnunua kwa mkopo mshambuliaji wa Chelsea na Ubelgiji, Romelu Lukaku, 30 na chaguo la pauni milioni 25.8 kumnunua mwishoni mwa msimu huu. ***(Telegraph)***

### TIMBER KUTUA ARSENAL

ARSENAL inakaribia kuwasajili beki wa Ajax na Uholanzi, Jurrien Timber, 22 na mshambuliaji wa Chelsea na Ujerumani, Kai Havertz, 24. ***(Sky Sports)***

### JONG NA MANCHESTER UTD

KLABU ya Manchester United bado ina nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Barcelona, Frenkie de Jong, 26, huku Bayern Munich pia ikichunguza uwezekano wa kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi. ***(90minutes)***

### AWANIWA WEST HAM

KLABU ya West Ham ipo kwenye mazungumzo na Juventus kuhusu mkataba wa kudumu wa kumnunua kiungo wa kati wa Uswizi, Denis Zakaria. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 alitumia msimu uliopita kwa mkopo Chelsea. ***(Sky Italia)***

### CAICEDO OFA BADO

KLABU ya Brighton bado hawajapokea ofa zozote kwa kiungo wa Ecuador, Moises Caicedo, 21 na wanamtaka kiungo wa kati wa Ajax na Ghana, Mohammed Kudus, 22. ***(Talksport)***

### CHIESA AWANIWA

LIVERPOOL na Newcastle United ni miongoni mwa klabu za Ligi Kuu ya England zinazomtazama fowadi wa Juventus mwenye thamani ya pauni milioni 51, Federico Chiesa, 25. ***(Corriere dello Sport)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# ARSENAL HAITAKI UTANI KWA DECLAN

**●●● Yatuma ofa ya tatu iliyoboreshwa ili kumng'oa nahodha huyo wa West Ham United...**

**LONDON,** England

ARSENAL imewasilisha ofa ya tatu kwa pauni milioni 105 kwa nahodha wa West Ham, Declan Rice ambayo sasa ni ya tatu.

**Mail Sport ilifichua Jumanne kwamba ofa ya tatu ya Washikabunduki hao ingefika ndani ya saa 48 na ofa iliyoboreshwa ya Arsenal kwa nahodha huyo inajumuisha fedha taslimu za uhakika za pauni milioni 100 pamoja na nyongeza ya pauni milioni 5.**

Ofa hiyo inazidi thamani ya West Ham ya pauni milioni 100 kwa nyota huyo wa England na, ikifaulu, itamfanya Rice kuwa uhamisho mkubwa zaidi kati ya klabu hizo mbili za England, ikiipita Manchester City iliyomnyakua Jack Grealish kwa pauni milioni 100 kutoka Aston Villa msimu wa joto wa 2021.

Habari za dau kubwa la Arsenal zinakuja baada ya ofa ya kwanza ya Manchester City kwa nahodha huyo wa wagonganyundo hao, ambayo ilikuwa ni pauni milioni 80 kama fedha taslimu za uhakika na nyongeza ya pauni milioni 10, kukataliwa rasmi Jumanne.

Huku hesabu ya West Ham sasa ikifikiwa na Arsenal, muundo wa mkataba huo utakuwa jambo kuu kuhusu iwapo ofa hiyo itakubaliwa.

West Ham wanapendelea sehemu iliyohakikishwa ya ada ilipwe ifikapo mwanzoni mwa 2025. Arsenal imekuwa ikitaka kulipa ada hiyo katika kipindi cha miaka mitano.

Baada ya kuona ofa mbili zimekataliwa, ofa ya awali ya Arsenal ilikuwa ya pauni milioni 75 pamoja na bonasi zaidi ya pauni milioni 15.

Manchester United pia wanavutiwa na Rice, lakini wanatazamwa kama washiriki wa mbio hizo.

United ingependelea kutumia wachezaji wa pembeni kama viboreshaji katika mpango huo; huku Harry Maguire na Scott McTominay wakivutiwa na kocha mkuu wa West Ham, David Moyes.

Tangu aanze kucheza kwa mara ya kwanza akiwa na umri wa miaka 18 mwaka 2017, Rice mwenye umri wa miaka 24 amekua shujaa wa nyumbani kwa klabu hiyo ya London Mashariki. Kwa jumla, amecheza mechi 245, akifunga mabao 15.

Rice - ambaye aliichezea Jamhuri ya Ireland mara tatu mwaka wa 2018 kabla ya kubadili uraia na kuuchukua wa England - amejidhihirisha kuwa mtu muhimu kwa vijana wa kocha Gareth Southgate, akicheza mechi 43.

Ushindi wa West Ham katika Ligi ya Europa Conference msimu uliopita ulihitimisha msimu uliokuwa mgumu kwa klabu hiyo.

# TEN HAG HANA UHAKIKA NA DE GEA



**MANCHESTER,** England

KUTOKUWA na uhakika kwa kocha Erik ten Hag kuhusu David de Gea kumechangia mabadiliko ya Manchester United juu ya mkataba mpya kwa mlinda mlango huyo wa Hispania.

Mail Sport ilifichua mapema mwezi huu kwamba mfumo wa mkataba mpya unaolenga kupunguza mshahara wa De Gea wa pauni 375,000 kwa wiki ulikubaliwa kati ya mchezaji huyo na klabu, lakini kutoridhishwa kwa Ten Hag juu ya kiwango cha namba moja wake huo kumeweka dili hilo hatarini.

Ripoti ziliibuka Jumanne zikidai kuwa De Gea alitia saini mkataba huo mpya kabla ya United kuunga mkono na kisha kuwasilisha ofa ndogo zaidi.

Mustakabali wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 pale Old Trafford sasa unaonekana kutokuwa na uhakika zaidi kuliko hapo awali ikiwa imesalia siku moja tu tu kabla ya kuwa mchezaji huru. Mkataba wake unamalizika Juni 30.

United bado wanaweza kumsajili tena De Gea baada ya tarehe hiyo, lakini inaonekana haiwezekani katika mazingira ya sasa. Huenda matokeo ni kwamba De Gea ataondoka baada ya miaka 12 ya kukaa United na kutafuta klabu mpya huku kukiwa na ofa nono kutoka kwa Saudi Arabia.

United wamefanya mazungumzo ya kiuchunguzi kuhusu mpango wa kumnunua Andre Onana wa Inter Milan kama mbadala wake, ingawa mazungumzo ya dau la pauni milioni 50 bado hayajafikiwa.

Maofisa wa klabu walikutana na wakala wa Onana, Albert Botines, wiki iliyopita kwa majadiliano juu ya uwezekano wa kumsajili.

Wachezaji kama vile mlinda mlango wa Porto Diogo Costa, David Raya wa Brentford na chipukizi wa Anderlecht Bart Verbruggen pia wametathminiwa na United.

# Spurs: Kane hauzwi bei yoyote

**LONDON,** England

HARRY Kane ameambiwa na Tottenham Hotspur kwamba hayupo kwa ajili ya kuuzwa msimu huu wa joto, vyanzo vimeiambia ESPN, licha ya Bayern Munich kuongeza nia ya kutaka kumnunua nahodha huyo wa England.

Imeripotiwa kuwa Bayern wamewasilisha ofa ya euro milioni 70 kwa Kane mwenye umri wa miaka 29, lakini vyanzo viliiambia ESPN kwamba Spurs haijapokea ofa rasmi kutoka kwa mabingwa hao wa Ujerumani.

Spurs wanafahamu nia ya Bayern kumnunua Kane, ambaye amebakisha mwaka mmoja katika mkataba wake katika klabu hiyo ya London, lakini hakuna mpango wa kumtoa fowadi huyo wakati wa dirisha hili la usajili.

Manchester United pia wanafuatilia hali ya Kane, lakini vyanzo vimeambia mara kwa mara ESPN kwamba haiwezekani kuhamia Old Trafford isipokuwa mchezaji huyo atalazimisha uhamisho kwa kuiambia Spurs kwamba anataka kuondoka msimu huu wa joto.

Kane ataweza kuondoka kama mchezaji huru mwishoni mwa msimu ujao ikiwa atachagua kutosaini mkataba mpya, na anaweza kuzungumza na timu Januari ili kufanya mazungumzo ya kuhama mwishoni mwa msimu ujao.





# Kovacic rasmi mali ya Man City

**MANCHESTET,** England

MANCHESTER City imekamilisha usajili wa kiungo, Mateo Kovacic kutoka Chelsea kwa mkataba wa miaka minne, washindi hao wa mataji matatu walitangaza juzi.

ESPN iliripoti mapema mwezi huu klabu hizo mbili zilikubaliana ada ya pauni milioni 25 kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 na nyongeza nyingine ya pauni milioni 5 na kiungo huyo wa kati wa Croatia na sasa amejiunga nao rasmi.

"Hii ni hatua nzuri kwangu, na siwezi kusubiri kuanza kuichezea na City," alisema Kovacic mara baada ya kukamilisha dili hilo la Man City.

"Yeyote ambaye ameitazama timu hii chini ya Pep anajua jinsi walivyo - kwangu, wao ni bora zaidi duniani. Mataji waliyoshinda ni wazi kwa wote kuona, lakini pia ni timu bora.

"Kujiunga na kikosi hiki ni ndoto kwa mwanasoka yeyote."

Kocha wa City, Pep Guardiola amekuwa na nia ya kuimarisha safu yake ya kiungo baada ya klabu hiyo kumkosa Jude Bellingham, ambaye alijiunga na Real Madrid mwezi huu, na nahodha Ilkay Gundogan aliyekamilisha uhamisho wa bure kwenda Barcelona Jumatatu.

"Mateo ni mwanasoka bora," mkurugenzi wa soka wa City Txiki Begiristain alisema. "Anaweza kucheza kama namba 6 au 8, ana uzoefu wa kutosha katika klabu za kiwango cha juu na anaelewa Ligi Kuu.

"Ulikuwa uamuzi rahisi sana kumleta City kwa sababu ana sifa za kimbinu na kiufundi tunazotafuta katika kiungo.

"Ni mtu ambaye tumemfuatilia kwa muda mrefu sana na kila mara tulivutiwa kila tulipomtazama."

HABARI MICHEZO

## Yanick Bangala awashusha presha mashabiki Yanga

INATOKA UKURASA 24

ufundi," alisema Bangala.

Aliongeza kuwa ana uhakika atapambana na kuwapa ushirikiano mkubwa makocha wapya ili kufikia malengo yao ikiwamo kutwaa mataji yote ya ndani na kuleta kombe la Afrika.

"Msimu huu tunataka kufanya vizuri zaidi na kwa kuwa tulifika fainali ya Kombe la Shirikisho basi malengo yetu itakuwa kutwaa ubingwa wa Afrika na kuleta kombe Tanzania, hii inawezekana tukiwa na malengo ya pamoja na kushirikiana vyema," alisema Bangala.

Baada ya ligi kumalizika, Bangala pamoja na Wakongo wenzake, Shaaban Djuma na Joyce Lomalisa walihusishwa kutaka kuondoka ndani ya klabu hiyo na kushinikiza uongozi uwaboreshee maslahi ili waendelee kuwamo kwenye kikosi cha Yanga msimu ujao.

## Simba SC kuanika majembe yake Jumatatu

INATOKA UKURASA 24

tangaza wachezaji wetu wapya, kazi imeanza kuelekea msimu ujao," alisema Ahmed.

Aidha, alisema kuhusu Onana ni kweli mchezaji huyo alikuja hapa nchini hivi karibuni na ameshaondoka.

"Onana ni mchezaji mzuri na ameshakuja Tanzania, tusubiri tuone kuanzia Jumatatu nani na nani watatangazwa kujiunga na Simba, sasa tuangalie kama atakuja Simba au hatokuja, wanachama na mashabiki wa Simba wavute subira, muda wetu ni ule ule saa saba mchana, jua kali dunia nzima inaona," alisema Ahmed.

Hata hivyo, licha ya Ahmed kutoweka wazi, taarifa zinasema tayari Simba imeshamalizana na winga huyo wa kushoto akitokea klabu ya Rayon Sport ya Rwanda.

Msimu huu, Onana alishika nafasi ya pili kwenye orodha ya wafungaji bora wa Ligi Kuu ya Rwanda, akipachika jumla ya mabao 10, akitanguliwa na wachezaji wawili, Robert Mukongotya wa Mukura Victory na Shaban Hussein Shabalala wa AS Kigali, wote wakiwa na mabao 12.



Kuhusu itakapoweka kambi msimu huu, Ahmed alikiri kuwa wanataka kuweka nje ya nchi, lakini itategemea na watatangaza pale Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF), litakapotoa ratiba yake ya msimu.

"Huwezi kuweka kambi kabla TFF kutangaza msimu mpya wa mashindano, ila tutakwenda nje," alisema.



# AZAM FC YAMWONGEZEA MKATABA NDOYE

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Azam FC umetangaza kumuongezea mkataba beki wake Pape Malickou Ndoye raia wa Senegal na sasa atasalia kwenye timu hiyo mpaka mwaka 2025.

**Mkataba wa awali wa beki huyo ulikuwa unamalizika mwakani na uongozi wa klabu hiyo umevutiwa na huduma ya beki huyo na kuamua kumuongezea mwaka mmoja kwenye mkataba wake wa sasa.**

Ndoye amekuwa mchezaji wa tano ndani ya kikosi cha Azam kutangazwa kuongezewa mkataba akitanguliwa na nyota wengine Sospeter Bajana ambaye amesaini mktaba wa miaka mitatu, James Akaminko, Nathaniel Chilambo ambao wote wameongeza mkataba wa miaka miwili huku Daniel Amoah akiongeza mkataba wa mwaka mmoja kama ilivyo kwa Ndoye.

Akizungumza na Mwandishi wa gazeti hili jana, Ofisa habari wa klabu hiyo Hasheem Ibwe, alisema wanaimarisha kikosi cha timu yao kwa sababu wamedhamiria msimu ujao kutwaa ubingwa na kufanya vizuri mashindano ya Kimataifa.

"Tunaimani na wachezaji wote tuliowaongezea mikataba kusalia ndani ya timu yetu, na hata nyota wapya tuliowasajili tuna imani na matarajio makubwa ya kutuwezesha kufanya vizuri na kutwaa mataji ambayo tumeyakosa kwa muda mrefu sana," alisema Ibwe.

Alisema uongozi wa timu hiyo umeamua kuhakikisha wanafanikiwa katika malengo yao na ndio maana wanafanya maboresho ya kikosi cha timu hiyo.




Vijana wakicheza mpira wa magongo katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## *Prisons yatoa 'Thank you' kwa wachezaji wake*

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Prisons nayo imeanza kufanya maboresho kwenye kikosi chake kwa kuanza kuwaondoa wale ambao hawahitajiki ili kuingiza wapya watakaokuja kuchukua nafasi zao.

Klabu hiyo imeachana na wachezaji wanne ambao ni Ramadhani Ntobi, Michael Masinda, Ismail Mgunda, huku ikimpeleka Shaaban Kisiga kwa mkopo kwenye klabu 'dada' Magereza ya Dar es Salaam.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Jackson Mwafulango amesema hayo yote yanafanyika kwa maagizo ya benchi la ufundi, hivyo wana uhakika kuwa watafanya vyema msimu ujao chini ya Kocha Mkuu Abdallah Mohamed 'Bares.'

"Uongozi wa Prisons unawashukuru waliokuwa wachezaji wetu, Ntobi, Masinda, Mgunda, Oscar na Kisiga kwa kuitumikia vizuri timu yetu msimu wa 2022/23, alisema Mwafulango na kuongeza,

"Kisiga yeye atacheza kwa mkopo katika klabu ya Magereza ya Ukonga Jijini Dar es Salaam msimu ujao na kuna mchezaji wetu golikipa Mussa Mbisa hajajiunga na klabu hiyo tangu alipopata majeraha mwezi Agosti mwaka jana katika mechi ya kwanza ya Ligi Kuu dhidi ya Singida Big Stars msimu uliomalizika, naye atajiunga na timu hiyo" alisema Mwafulango.

Alisema mpaka sasa wameachana na wachezaji wanne tu ambao hawatokuwa sehemu ya timu kwa msimu ujao ingawa zoezi bado linaendelea.

"Uongozi kwa kushirikiana na benchi la ufundi unaahidi kufanya usajili mzuri ambao utaongeza chachu ya ushindani katika timu yetu na kuifanya kuwa tishio msimu wa 2023/24," alisema Mwafulango.

Tanzania Prisons msimu uliopita imemaliza ligi ikiwa katika nafasi ya nane.

Michezo
Alhamisi Juni 29, 2023
Nipashe



Ten Hag hana uhakika na De Gea UKURASA 22



Yanick Bangala

# Simba SC kuanika majembe yake J'tatu

**Na Adam Fungamwango**

UONGOZI wa klabu ya Simba umesema sasa wapo tayari kuanza kuwatambulisha wachezaji wake wapya waliowasajili kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu na mashindano ya kimataifa.

Simba itaanza kuwatangaza wachezaji hao Jumatatu ijayo lakini imekiri kufanya mazungumzo na winga Mcameroon, Leandre Willy Onana Essomba anayetegemewa kujiunga na timu hiyo kwa ajili ya msimu ujao.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, amesema kuwa wiki hii wanataka kumalizana na wachezaji wote ambao wataondoka, pia kupisha sikukuu ya Idd el Haji, kabla ya kuanza kuanika majembe yao kuanzia Jumatatu.

"Kuanzia Jumatatu tunaanza kuangusha mmoja mmoja kama mkwezi anavyoangusha nazi akiwa juu ya mnazi, huwa anaangusha moja baada ya nyingine, kwa hiyo tusubiri, tuwe na subira, tule kwanza Idd, tuchinje, Jumatatu tukiamka, tutaanza kuwa-

INAENDELEA UKURASA 23



Leandre Willy Onana Essomba

# BANGALA AWASHUSHA PRESHA MASHABIKI YANGA

## Asema bado ana mkataba wa mwaka mmoja na mabingwa hao, aahidi kujituma na kushirikiana...

**Na Saada Akida**

BAADA ya tetesi kuwa huenda kiungo wa Yanga, Yanick Bangala, atatimka kwenye kikosi cha timu hiyo, nyota huyo amesema bado ataendelea kuwapo Jangwani kwa kuwa ana mkataba mmoja zaidi na mabingwa hao wa soka nchini.

Bangala pamoja na nyota wengine wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ndani ya Yanga, alikuwa akihusishwa kutaka kuondoka ndani ya timu hiyo huku akihusishwa kutaka kujiunga na matajiri wa Chamazi, Azam FC.

Akizungumza na Nipashe jana, Bangala alisema, anawashukuru mashabiki wa Yanga kwa sababu siku chache zilizopita yaliibuka mengi kuhusu hali yake na klabu hiyo anayoitumikia lakini bado alikuwa imara na kuweka imani yao kwa timu.

> **"Yamesemwa mengi sana, lakini nawahakikishia wanayanga mimi bado nina mkataba na klabu yangu mpaka mwakani, nitaendelea kuheshimu mkataba wangu," alisema Bangala.**

Alisema anafahamu kipindi hiki cha usajili na yatazungumzwa mengi sana juu ya mustakabali wa wachezaji lakini yeye bado ni mchezaji halali wa Yanga na yupo tayari kuitumikia msimu ujao.

"Nimewekeza nguvu na akili zangu kwa asilimia 100 kuhakikisha tunafikia malengo yetu, tulifanya vizuri msimu uliomalizika na sasa tunajiandaa kwa ajili ya msimu ujao binafsi nitakuwa bega kwa bega na benchi jipya la

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002